epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Agosti 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581755
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**YORO AZUA HOFU MAN UNITED**

UKURASA WA 3

**KIKWETE ASIMULIA ALIVYOPATA UGUMU KURUHUSU MKEWE KUGOMBEA UBUNGE**

UKURASA WA 3

**GUMZO LATANDA NGEDERE, BUNDI KUATHIRI SAFARI TRENI YA SGR**



UKURASA WA 4

RIPOTI MAALUM -2

**UHABA WALIMU ULIVYO JANGA SUGU LA TAIFA**

# Serikali yaahidi ajira 137,000 sekta afya

UKURASA 2

UKURASA WA 22

**DI MARIA: VITISHO VIMENIZUIA KUICHEZEA ROSARIO**



KIUNGO wa kati wa Argentina, Angel Di Maria, amesema alikuwa tayari kurejea katika klabu ya nyumbani...



## Mbaroni madai ya kubadilisha fedha kigeni bila kibali

UKURASA 3



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akitoa Tuzo ya Mkapa ya Uongozi Thabiti kwa mmoja wa washindi mbalimbali kutoka sekta ya afya nchini, wakati wa kilele cha Kumbukizi ya Tatu ya Urithi wa Mkapa Dar es Salaam jana. Wengine ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na Mjane wa Hayati Benjamin William Mkapa, Mama Anna Mkapa. **PICHA: IKULU**



## Daktari aanika maumivu upasuaji wagonjwa watumiaji wa bangi, pombe

UKURASA 2

MICHEZO GAMONDI AKOSHWA NA UBORA WA MZIZE UK.24 KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Dk. Samia Suluhu Hassan akimvalisha Kamishna wa Magereza, Jeremiah Yoram Katungu, cheo kipya cha Ukamishna Jenerali wa Magereza (CGP), kabla ya kumwapisha kuwa Mkuu wa Jeshi hilo, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali yaahidi ajira 137,000 sekta ya afya

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali ina mpango wa kuajiri wahudumu wa afya 137,000 na tayari mchakato wa kuwapata umekamilika ngazi ya halmashauri.

Amesema mafunzo ya kundi la kwanza yameanza mwezi huu (Julai) katika vyuo vya afya nchini.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifunga kumbukizi ya tatu ya Hayati Benjamin Mkapa iliyoandaliwa na Taasisi ya Benjamin Mkapa na kuhudhuriwa pia na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kumbukizi hizo zimehudhuriwa pia na viongozi wa serikali, wastaafu na wake wa viongozi wakuu wastaafu wakiongozwa na mama Anna Mkapa.

Rais Samia alitaja hatua nyingine za kutengeneza ajira kwa watumishi kada ya afya kuwa ni ziara zinazofanyika nchi mbalimbali kuzungumza nazo kama zina uhitaji huo wawachukue.

"Nilikuwa ninazungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi hii kwamba, kundi la kwanza la wauguzi 200 kwa kushirikiana pia na taasisi hii tayari wameshakwenda na wameanza kazi na tunatengeneza kundi la pili," alisema.

Rais Samia aliitaka Ofisi ya Waziri Mkuu iimarishe timu ya kuratibu rasilimali katika sekta ya afya ili ifanye kazi zake.

Kadhalika aliitaka Wizara ya Afya kukamilisha utafiti wa kitaifa kubainisha hali halisi ya wataalam wa afya walioko soko la ajira na kufahamu nguvu kazi iliyoko nje katika vituo vya tiba.

Pia, aliitaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutengeneza mkakati wa diplomasia ya afya na kusaidia upatikanaji wa nafasi za mafunzo ya juu ya utaalam kwa watumishi wa sekta hiyo.

Alisema amezungumza na Mtendaji wa Global Education Link (GEL) ambaye amemweleza kwamba, wanazungumza na vyuo duniani ili kupeleka wanafunzi fani za afya kwa fedha ambazo zingelipwa ndani ya nchi.

Alisema urithi alioacha Benjamin Mkapa unafanya aendelee kuishi hata baada ya kifo chake.

Alisema miaka minne tangu atangulie mbele ya haki, Mzee Mkapa anakumbukwa kama baba wa taasisi, mifumo na wa mageuzi, na alitumia muda mwingi wa hotuba zake kuelezea mambo hayo matatu katika sekta zote.

"Ndio maana wadau wengi wa maendeleo wameelekeza nguvu zaidi kudhibiti maradhi ya kuambukiza na kidogo kwenye miundombinu ya afya. Ni ukweli kwamba mafanikio yake yanategemea watumishi wa afya wa kutosha na wenye weledi," alisema.

Rais Samia alisema kujenga kituo cha afya inaweza kukamilika ndani ya mwaka mmoja ikiwa fedha zipo wakati inahitajika miaka sita kumwandaa daktari mmoja na walau miaka mitatu kumwandaa muuguzi huku dakati bingwa huchukua miaka tisa hadi 12.

Alisema kupoteza mtumishi mmoja sekta ya afya ni hasara kubwa kwa taifa, kulinganisha na uwekezaji mkubwa wanaofanya.

"Ninapozunguka mikoani changamoto namba moja ninayokutana nayo ni ya watumishi katika sekta ya afya na elimu. Kwa nini sekta hizi, idadi ya watu inakua kwa haraka, tunazaliana mno na mahitaji ni makubwa mno. "Ajira zinaendana na ukuaji uchumi tukipata nafasi kidogo uchumi ukikua kidogo hapo hapo tunasema sekta ya afya na elimu," alisema.

Aidha, alisema changamoto ya upungufu wa watumishi imesababisha serikali kutanua wigo ufadhili wa masomo mikopo ya elimu ya juu.

Rais Samia alisema takwimu zilizotolewa katika mkutano huo zinaonesha kuna upungufu wa asilimia 60 na kueleza kwamba, kuna jitihada za kuajiri watumishi wengi kwa miaka mitano.

Alisema taasisi za kidini zinajitahidi kuingia sekta ya afya ingawa wafanyakazi wa hospitali hizo mategemeo ni serikalini.

"Wengi wamejikita katika utoaji huduma na katika miradi ya afya kwa jamii, kutengeneza nguvu kazi ni mzigo wa serikali peke yake, zikijipanua tunakuwa na mzigo mkubwa wa wafanyakazi," alisema.

Aliihakikishia BWF na taasisi zingine kwamba, kadri serikali inavyotoa ajira wataalam wa afya wa mkataba walioko kazini wataendelea kuhuhishwa katika ajira za serikali.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye ni Msarifu wa Taasisi ya BMF, alisema kuwapo kwa taasisi hiyo kumechangia nguvu kazi ya rasilimali watu

Alisema kwa upande wa Zanzibar wanaendelea kujenga miundombinu ya afya na kuendelea kutoa ajira na kuboresha mazingira ya kazi kwa kujenga nyumba za watumishi wa afya.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema serikali imeongeza posho za madaktari anapoitwa nje ya saa za kazi, posho za sare za wauguzi na ile ya kuchunguza maiti kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini BMF, Dk. Adeline Kimambo, alisema Mpango Mkakati wa miaka sita (2024/30) wa Taasisi hiyo uliozinduliwa juzi, pamoja na mambo mengine umelenga kuimarisha afya na ustawi wa jamii nchini na nje ya nchi ambao pia, utaongeza watanzania wengi kuwa na bima ya afya.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo, Dk. Ellen Mkondya- Senkoro, alisema Hayati Mkapa amewaachia urithi mwingi ambao unatakiwa kuendelezwa kizazi hadi kizazi, akishukuru familia yake, kupitia mke wake, Anna Mkapa, kuwaamini na kumega sehemu ya urithi wa familia kwa ajili ya watanzania.

Akitoa salamu za familia ya Hayati Mkapa, William Erio, alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kumtunza mama Mkapa na wadau waliofanikisha kumbukizi hiyo.

# Daktari aanika maumivu upasuaji wagonjwa wanatumia bangi, vilevi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

DAKTARI Bingwa wa Usingizi wa Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa, Dk. Venance Misago, ameanika machungu wanayopata wagonjwa wanaotumia vilevi kama pombe na bangi, wakati wa kufanyiwa upasuaji.

Amesema baadhi ya wagonjwa wamekuwa wakipata maumivu kutokana na dawa wanazopewa kutokuwa na uwezo wa kudhibiti hali ya vilevi mwilini kwa kuwa zinawasumbua.

Kwa mujibu wa daktari huyo, kutokana na matumizi ya muda mrefu ya pombe, mgonjwa anakumbana na maumivu makali na wakati mwingine baadhi wanalia na kutoa malalamiko kuhusu wanavyoumia hali ambayo huwa ngumu kufanyiwa upasuaji kama inavyotarajiwa.

Kutokana na hali hiyo, ameshauri wanaotumia vilevi kama kutoa taarifa kabla ya huduma ya upasuaji ili wapewe aina ya dawa za maumivu kulingana na mahitaji.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe jana, Dk. Misago alisema taarifa hiyo itasaidia madaktari kumpa dawa itakayomfanya asipate maumivu, tofauti na akikaa kimya atapokutana na maumivu makali wakati upasuaji unaendelea.

"Dawa za usingizi tunazowapa zinatofautiana. Anayetumia vilevi vikali kwa muda mrefu unaweza kumpa dawa na bado akaendelea kuwa na maumivu kwa kuwa dawa ya usingizi tunayompa haimsaidii lakini akisema tunajua tumpe ya aina gani ndiyo maana mgonjwa huulizwa kabla ya huduma," alisema.

Pia alisema aina za dawa za usingizi wanazotoa kwa wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji zinapaswa kumfanya mgonjwa asisikie maumivu wakati wa upasuaji lakini wamekuwa wakikutana na wengi ambao husikia maumivu hasa wenye umri mkubwa wenye historia ya kutumia vilevi vikali.

Dk. Misago alibainisha kuwa mgonjwa anayetumia bangi na vilevi vikali ni vigumu dawa ya usingizi kufanya kazi kwa sababu kilevi alichotumia kinashindana na dawa inayoingia kwenye mwili wa mgonjwa.

Alisema ameshakutana na kesi kadhaa ambapo wakati upasuaji unaendelea baadhi ya wagonjwa wanakuwa wanalia na kulalamika kutokana na maumivu makali na wakimuuliza wanatoa majibu ya kuwa hutumia vilevi vikali.

Kwa mujibu wa mtaalam huyo, baada ya kukutana na kesi hizo, wameamua kutoa elimu kwa wagonjwa kabla ya kufanyiwa upasuaji kwa kuhojiwa kwa kina ili daktari awe na taarifa za awali za aina ya vinywaji wanavyotumia ili ajue aina na kiasi cha dawa ya kumpatia.

Alisema endapo mgonjwa anatumia bangi na vilevi vikali ni rahisi kupata maumivu wakati wa upasuaji kutokana na dawa ya usingizi aliyopewa inashindwa kufanya kazi.

"Tunaomba mgonjwa akiletwa hospitali ni vyema yeye au ndugu zake wakaeleza aina ya vilevi anavyotumia ili kuwasaidia madaktari kutoa dawa stahiki ya usingizi kulingana na hali yake," alisema.

Dk. Misago alisema mtu anapoingia chumba cha upasuaji kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji ni muhimu kueleza historia yake, ili wataalamu wajue jinsi ya utoaji tiba kulingana na maelezo yake.

Kuhusu maumivu na jinsi ya kuyadhibiti, alisema ili kukabiliana na changamoto hizo, ni muhimu mgonjwa kueleza aina ya dawa, vinywaji au vilevi anavyokuwa unatumia kwa muda mrefu.

"Hii itasaidia kujua jinsi ya kudhibiti maumivu utakayopitia wakati unapopatiwa huduma au upasuaji unapoendelea. historia ya mgonjwa ina umuhimu mkubwa kwa wataalam kudhibiti maumivu kabla, wakati na baada ya upasuaji.

"Mfano; mgonjwa alikuwa anatumia pombe kali au sigara haramu ya bangi ni muhimu kueleza ili kujua aina ya dawa za kumpatia ambazo zitadhibiti maumivu wakati wa upasuaji," alisema.

## Kikwete asimulia alivyopata ugumu kuruhusu mkewe kugombea ubunge

**Na Gwamaka Alipipi,** LINDI

RAIS Mstaafu, Jakaya Kikwete, amesimulia alivyopata ugumu kumruhusu mkewe, Salma Kikwete, kugombea ubunge katika Jimbo la Mchinga mkoani Lindi.

Amesema alimruhusu kwa shingo upande kuingia katika kinyang'anyiro hicho baada ya kufuatwa na wazee 15 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoka Mchinga waliotaka aridhie.

Kikwete alisema hayo jimboni Mchinga wilayani Lindi katika mkutano wa hadhara wa Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ambaye yuko katika mikoa ya Kusini akifanya ziara ya kuimarisha na kukijenga chama.

Alisema wazee hao walimweleza kwamba wamechoka kuongozwa na mbunge kutoka chama cha upinzani na kwamba mtu pekee anayeweza kumng'oa mbunge huyo ni Mama Salma.

"Nakumbuka wazee 15 walinifuata wakitoka Mchinga wakasema tunamtaka mke wako agombee Jimbo la Mchinga. Tunaomba ukubali kisha umshawishi akubali. Nikawajibu kwamba siwezi kwenda kumshawishi kwa sababu ni lazima aridhie kutoka moyoni. Pia nikawauliza je, mmejiandaa msije mkamfedhehesha akashindwa. Wakanijibu wamejiandaa," alisema.

Kikwete alisema alikubali ombi la wazee hao kwa shingo upande, kisha akamfuata mkewe (Salma) na kumweleza aliyoambiwa na wazee. Pia alisema alimweleza mkewe ajipime kama anaweza kugombea ubunge na endapo yuko tayari kupambana.

"Baada ya kumweleza hayo alinijibu kwamba endapo nikimuunga mkono atashiriki kugombea ubunge jimbo hilo," alisema.

Baada ya kauli hiyo, alisema alilazimika kumuunga mkono katika kampeni za kugombea ubunge, kwamba alishiriki kwa asilimia 100 wakati wa uzinduzi.

Hata hivyo, Kikwete alimhakikishia mkewe ataendelea kumuunga mkono wakati wote kama anavyoipa ushirikiano CCM na kwamba asiwe na wasiwasi.

**NCHIMBI AMTAJA**

Naye Dk. Nchimbi alimtaja Dk. Kikwete kuwa mmoja wa wa viongozi waliomfundisha kuwa na nidhamu na uwajibikaji kwa wananchi.

Nchimbi alitoa mfano kwamba mwaka 2002 aligombea ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM lakini alishindwa.

"Baada ya kura zangu kutokutosha siku kadhaa baadaye nikiwa kwenye shughuli fulani, nilikutana na Rais Benjamin Mkapa nikamwambia nimeshindwa katika uchaguzi NEC lakini nitashiriki uchaguzi wa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM mwakani (mwaka uliofuata) na nitashinda," alisema Dk. Nchimbi.

Alisema baada ya kuzungumza hayo na Mkapa kesho yake Kikwete alimfuata na kumwambia kwamba kauli aliyomweleza Rais Mkapa si nzuri, kwamba inamaanisha lazima atashinda.

"Nakumbuka Kikwete aliniambia napaswa kuwa na nidhamu. Pia aliniambia nilipaswa kusema kwamba mwakani nitashiriki uchaguzi wa UVCCM na endapo chama kitaridhia nitakuwa mshindi," alisema Dk. Nchimbi.

Alisema hata aliposhinda uchaguzi huo, Kikwete alimfuata tena na kumwambia asijione bora kuliko wengine na asiwasahau aliowashinda hususani aliyeshika nafasi ya pili.

"Ninawaambia leo yule aliyeshika nafasi ya pili, Frank Uhahula sijamtupa hivi sasa ni msaidizi wangu masuala ya protokali (itifaki)". Pia alisema Kikwete alimfundisha kuwa mtu wa kuwajibika katika jamii.

Dk. Nchimbi alitoa mfano alipokuwa Rais (Kikwete) alimteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kukatokea tatizo la usalama katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

"Siku moja nilizima simu ili nipumzike maana nilikuwa nimetoka safari nimechoka. Ilipofika saa 9:00 usiku magari matatu yalikuja nyumbani kwangu. Mtu mmoja alishuka na kuingia ndani kwangu akanipa simu akaniambia Rais anataka kuongea na wewe.

"Nilipopokea, Rais Kikwete aliniambia nimekupa jukumu la kusimamia usalama wewe unazima simu. Kisha akakata simu," alisema na kubainisha kwamba baada ya hapo alijawa na hofu akidhani kwamba muda wowote uteuzi wake utatenguliwa, lakini haikutokea hivyo.

Alisema kutokana na kitendo hicho alijifunza kwamba kiongozi akiwa na wajibu kwa jamii hapaswi kuzima simu bali anapaswa kuwa makini muda wote.

# Mbaroni madai ya kubadilisha fedha kigeni bila kibali

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Arusha kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), limemkamata mfanyabiashara Samwel Mbise (42), mkazi wa Sanawari kwa tuhuma za kubadilisha fedha za kigeni bila kibali.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma, iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, SACP Justine Masejo, mtuhumiwa huyo alikamatwa Julai 29, mwaka huu.

Mtuhumiwa huyo alikutwa na fedha za nchi mbalimbali na hakuwa na kibali cha BoT cha kufanya biashara hiyo kisheria.

Kamanda Masejo alitaja fedha hizo kuwa ni Dola za Marekani 5,952, Euro 835, Dola za Canada 1,845, Paundi za Uingereza 45, Franc za Uswis 20.

Nyingine ni Dola za Australia 50, Qatar Riyals 05, Paundi za Misri 25, Shilingi za Kenya 38,400 na Shilingi za Tanzania 52,552,000 ambazo jumla yote ni fedha za Kitanzania 75,809,649.

Jeshi hilo linaendelea kumhoji mtuhumiwa huyo, upelelezi utakapokamilika jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

Aliwataka wafanyabiashara kufuata sheria za BoT kuhusu kubadilisha fedha za kigeni ambazo zimeainishwa kisheria.

**KANUNI**

Kwa mujibu wa kanuni za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni za mwaka 2023, zilizotolewa kwenye Tangazo la Serikali namba 729 la Oktoba 6, 2023, zimeweka masharti;

Katazo la kufanya biashara bila leseni, vigezo, maombi ya leseni, jina la biashara, idhini ya awali, mapitio ya uamuzi wa benki kukataa maombi, masharti baada ya idhini ya awali, ukaguzi kabla ya kuanza biashara, utoaji na uhalali wa leseni, ada ya mwaka, mabadiliko ya umiliki, matakwa ya mtaji, kufungua tawi na kuhamia duka la kubadilisha fedha Daraja A.

Kanuni hizo zinaelekeza maombi ya leseni ya duka la kubadilisha fedha za kigeni ya hoteli, muundo wa uteuzi wa wajumbe wa bodi na wakurugenzi wakuu, majukumu ya bodi, muundo na udhibiti wa ndani, wigo wa uendeshaji, uhamisho wa biashara.

Pia kuonyesha viwango vya kubadilisha fedha, ada, tangazo, na leseni, shughuli, amana ya dhamana, akaunti ya wateja, katazo la miamala isipokuwa ya papo kwa papo, kukataa kuuza, uuzaji wa fedha za kigeni kwa wasio wakazi.

Aidha, kanuni hizo zinaweka taratibu za utumaji wa fedha kimataifa, taarifa za chanzo na madhumuni ya fedha za kigeni, ukusanyaji, uwasilishaji na uhifadhi wa data, utambuzi na utoaji wa taarifa za miamala shuku, usiri wa miamala.

Eneo jingine ni taarifa za fedha, ukaguzi, mafunzo, kufunga biashara kwa hiari na kusalimisha leseni, adhabu za kiutawala, notisi ya kusitisha au kufuta leseni na kufutwa.

"Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni za Mwaka 2023. Zitatumika kwa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yaliyopatiwa leseni na Benki Kuu ya Tanzania kufanya biashara Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar," ilisema sehemu ya kanuni hizo.



Mkazi wa Kijiji cha Maduma, Kata ya Kwabada, wilayani Muheza mkoani Tanga, Adriano Thomas (36) akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, baada ya kuhukumiwa kifungo cha jela maisha na Mahakama ya Wilaya ya Muheza hivi karibuni, kwa kosa la kumbaka mtoto (9) wa darasa la kwanza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Gumzo ngedere, bundi kuathiri safari ya SGR

**Na Romana Mallya**

HITILAFU ya umeme iliyotokea kati ya stesheni za Kilosa na Kidete mkoani Morogoro na kusababisha treni ya reli ya kiwango cha kimataifa (SGR) kusimama kwa muda wa saa mbili, imeibua mjadala mzito mtandaoni.

Mjadala huo uliibuka baada ya Shirika la Reli Tanzania jana kueleza kwamba taarifa za awali zinaonyesha hitilafu za aina hiyo husababishwa na wanyama kama ngedere au ndege aina ya bundi.

Kutokana na sababu hiyo, wadau wamerejelea kauli iliyowahi kutolewa Mei, 2020 na Mkurugenzi Mkuu wa (TRC), Masanja Kadogosa, kwamba treni hizo zitakuwa na uwezo wa kutumia mafuta, lakini zina uwezo wa kuhifadhi umeme endapo utakatika.

Katika mitandao ya kijamii, baadhi walichukua picha ya bundi na ngedere na kuwavika vikoti vya kuakisi mwanga wakionekana wako kwenye mitambo ya reli wakiwa wameshikilia vifaa vya kukatia umeme wakati treni ikiendelea na safari.

Utani mwingine mtandaoni ni unaonyesha picha ya treni na juu yake kukiwa na ngedere na bundi ikiwa na maelezo yanasomeka: "Ngedere na bundi wakatiza usafiri wa SGR nchini Tanzania."

Picha nyingine ilimwonesha ngedere akiwa juu ya jiwe msituni huku maelezo yake yakisomeka "Niache kula matunda porini nije kuchezea umeme wenu mnaumwa nyie?"

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa TRC, Jamila Mbarouk, ilisema hitilafu hiyo ya umeme ilijitokeza juzi kati ya stesheni za Kilosa na Kidete mkoani Morogoro.

Taarifa hiyo ilisema hitilafu hiyo ilisababisha treni ya SGR iliyokuwa na abiria ikitokea Dar es Salaam kwenda Dodoma kusimama kwa muda wa saa mbili.

"Taarifa za awali zinaonyesha kuwa hitilafu za aina hiyo husababishwa na wanyama (ngedere) au ndege (bundi) wanapogusa nyaya za umeme zilizotandazwa juu ya reli.

"Hitilafu ilisababisha umeme kukatika katika kituo cha kupooza umeme namba saba (Godegode) ambayo kitaalamu hujulikana kama (Instanteneous Overcurrent Protection Trip) majira ya saa 4:20 usiku," alisema Mbarouk katika taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema mafundi wa TRC walitatua changamoto hiyo na kurejesha umeme saa 6:30 usiku na treni hiyo kuendelea na safari kwenda Dodoma na kuwasili saa 7:57 usiku.

Kutokana na tatizo hilo, TRC imeomba radhi wateja kwa usumbufu uliojitokeza.



CAG wa zamani, Prof. Mussa Assad

# Uhaba wa walimu janga sugu la taifa

**Na Halfani Chusi**

**HII ni sehemu ya pili ya ripoti inayoangazia hali ya rasilimali watu katika shule za msingi nchini. Katika sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na ushuhuda wa uhaba mkubwa wa walimu katika Shule ya Msingi Lituhi, wilayani Nyasa. Endelea...**

Mwanafunzi wa darasa la saba katika shule hiyo, Jackson Jolamu, anasema upungufu wa walimu unasababisha baadhi ya wanafunzi kukosa vipindi na wengine kutofaulu vizuri mitihani.

Jolamu pia analalamikia upungufu wa matundu ya choo shuleni, akidai baadhi ya wanafunzi wamekuwa wanaugua magonjwa anayoambukizwa kwa njia ya haja ndogo.

Mwanafunzi huyo pia anasema upungufu wa madawati shuleni unasababisha washindwe kuandika vizuri na "kujisomea kwa nafasi".

Mwananfunzi mwingine wa shule hiyo, Immaculate Joseph, anaungana na kaka yake Jolamu kwamba changamoto tajwa ni kikwazo kwao kufanya vizuri kitaaluma.

"Tunashindwa kumaliza mada kwa wakati, tunalazimika kuja shuleni Jumamosi kufidia siku tulizokosa masomo.

"Matundu ya vyoo machache, Tunapata shida tunapokwenda kujisaidia kwa sababu tupo wengi. Kama umebanwa sana unapata shida maana wakati mwingine kunakuwa na foleni... (alitamka neno lenye maana ya msalani)," Immaculate analalama.

Mwalimu wa Taaluma shuleni huko, Elfrida Kilumbo anasema upungufu wa walimu unasababisha wanafunzi wengi kuwa watoro, akieleza uzoefu wake hata kuwamudu inakuwa shida.

"Vyoo vilivyopo ni vichache, maji yenyewe ni shida, hakuna maji. Wanafunzi wanalazimika kuyafuata mbali, ndio hayo tunayatumia kusafisha vyoo. Madawati machache watoto wengi wanaketi chini, hawaandiki vizuri, wakati mwingine wanachafua nguo kutokana na vumbi.

"Darasa la tatu na la pili wanaketi chini, sasa ukiangalia mtoto anatoka la kwanza alikuwa anakaa kwenye dawati, anaingia la pili anakaa chini, tayari hali hiyo inampunguzia ile morali ya kusoma na kuandika vizuri," anasema

Mwalimu Elfrida anaomba serikali kutatua changamoto zinazokamisha maendeleo ya wanafunzi kitaaluma na kujenga nyumba walau nne kwa ajili ya walimu wa shule hiyo ili waishi jirani na kituo cha kazi na kuepuka kulipa kodi ya pango.

"Hii itachangia walimu wanaokuja kufanya kazi, wawe na bidii kazini na kutotamani kuhama mapema kama ilivyokuwa kwa walimu wengine waliopita.

"Vyoo vya walimu vinatosha, hata vyumba vya madarasa vipo vingi, mpaka vingine havitumiki tungekuwa na madawati mengi na walimu, wanafunzi wangesoma kwa raha sana," anasema Elfrida.

Ernest Milinga mmoja wa wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo, anashangaa kuona shule hiyo ina upungufu wa walimu, ilhali ni shule mama na ipo katikati ya kijiji, ikitegemewa na wanafunzi wote wa eneo hilo.

Mkazi mwingine wa kijiji Lituhi, Charo Komba anashauri serikali kuajiri walimu kuziba mapengo ya waliohama na kustaafu.

"Ninaomba kupitia gazeti hili taarifa ifikie viongozi wengine, mwezi wa saba (Julai) mwaka huu, kuna mwingine anastaafu, watabaki watano, maana Mwalim Mkuu huwezi kumhesabu kwa sababu anakuwa na ratiba nyingi nje na kufundisha.

"Inafika mahali hatutamani kuitwa Watanzania kwa sababu hatuoni faida tunatamani tungekuwa Wamalawi kwa sababu tupo kijiji cha mwisho kufika huko.

"Sera ya elimu imekaa vizuri kwa mijini lakini si huku kijijini, walimu wanastaafu hakuna wanaokuja kama mbadala, tunaomba serikali itusaidie kutatua matatizo yanayokabili shule yetu," anasema.

Mbunge wa Nyasa, Stella Manyanya, anasema uhaba wa walimu unafanya wanafunzi wakose haki yao ya msingi ya kupata elimu bora.

"Shule za huku pembezoni walimu ni wachache sana, serikali haichukui hatua. Wakianza kuajiri wanawajaza mijini, ninashauri tuchukue walimu ambao wanatoka maeneo ya hukuhuku vijiji vingine.

"Kama ni mwalimu wa Lituhi, akafundishe huko. Hawa hawawezi kuhama kwa kisingizio cha mazingira magumu kwa sababu huku ndiko kwao," anashauri mbunge huyo.

Kimsingi, kinachoshuhudiwa shuleni Lituhi, si tu kinakinzana na maelekezo ya kisera, bali pia ni ishara ya kutotekelezwa kikamilifu hoja ya CAG ya mwaka 2017 kuhusu miundombinu na samani shuleni.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania ya Machi 2017, CAG (kipindi hicho Prof. Mussa Assad) alibaini kuwapo uchakavu mkubwa wa miundombinu na samani za shule za msingi nchini, akipendekeza serikali iboreshe samani na miundombinu iliyopo na kujenga mipya, pia iongeze rasilimali watu.

> **"Matundu ya vyoo machache, Tunapata shida tunapokwenda kujisaidia kwa sababu tupo wengi. Kama umebanwa sana unapata shida maana wakati mwingine kunakuwa na foleni... (alitamka neno lenye maana ya msalani)," Immaculate analalama.**

Vilevile, katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu, CAG Charles Kichere, anasema amebaini halmashauri za wilaya 13 alizozikagua, zina uhitaji wa walimu 24,609 wa shule za msingi, lakini zinao walimu 14,622, hivyo kuwa na upungufu wa walimu 9,987 (asilimia 41).

"Upungufu wa walimu unatokana na serikali kutoajiri idadi ya kutosha ya walimu, sambamba na ongezeko la idadi ya wanafunzi, kupungua kwa idadi ya walimu kunakotokana na kustaafu katika utumishi wa umma,

vifo, na kuacha kazi kwa sababu mbalimbali kama vile mazingira yasiyovutia katika kufanya kazi, ujira usivutia na kukosekana motisha.

"Upungufu wa walimu niliobaini katika mamlaka 13 za serikali za mitaa una athari za moja kwa moja katika ufaulu duni wa wanafunzi wa shule za umma.

"Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais- Utumishi na Utawala Bora, ipeleke walimu katika shule zilizoathirika

zaidi na upungufu.

"Aidha, serikali inashauriwa kuweka juhudi zaidi

katika kuboresha mazingira ya kufundishia kwa kujenga nyumba za watumishi, madarasa na kusambaza vifaa vya kufundishia, kuboresha

stahiki za walimu kama mishahara, kulipa madeni na kutoa motisha ili kuvutia walimu kuendelea na utumishi," CAG anawasilisha hoja yake.

HABARI KITAIFA

## Dola inavyoathiri ujenzi wa nyumba

**Na Beatrice Moses**

KUYUMBA kwa bei ya dola kumezua changamoto katika miradi ya ujenzi, kwani imesababisha kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investment (WHI) Dk. Fred Msemwa, alisema hayo juzi Dar es Salaam kwenye hafla fupi ya kutia saini mkataba na Kampuni ya Shandong Hi-Speed Dejian Group ujenzi wa mradi wa nyumba 101 Mikocheni, zitakazouzwa kwa mkopo kwa watumishi wa umma.

"Kutokana na kuyumba kwa bei ya dola nyumba hizi zikikamilika zitakopeshwa kwa Sh.milioni 99 kwa bei ya chini na bei ya juu itakuwa Sh.milioni 234 ikiwa ni nyumba yenye vyumba vitatu vya kulala, bei hiyo ingepungua kwa asilimia 10 kwa kila nyumba hizi kama bei ya dola ingekuwa imetulia," amesema Dk. Msemwa.

Mradi huo unaogharimu Sh. bilioni 18 unahusisha ghorofa 12 unatajwa kuwa ni wa kisasa na utajengwa ukihusisha teknolojia inayotumika kweye viwango vya ujenzi vya kimataifa, utakamilika ndani ya miezi 18.

Dk. Msemwa alisema mradi wa ujenzi wa nyumba hizo ni sehemu ya ujenzi wa nyumba 218 zinazotarajiwa kujengwa na WHI katika maeneo tofauti nchini, hadi sasa nyumba 1,003 zimeshajengwa kwenye mikoa 19, ambapo wafanyakazi wa umma na wengine wa mashirika binafsi ambao ni wanachama wa mifuko ya hifadhi wameuziwa kwa kukopeshwa.

Msaidizi Mtendaji wa Mkurugenzi wa Shandong Hi-Speed Dejian Group, Michael Meng, alisema watajenga mradi huo kwa kuzingatia makubaliano ili kuhakikisha jengo hilo linakuwa salama kwa matumizi yaliyokusudiwa .

Mkurugenzi wa Ushauri na Ubunifu, Sephania Solomon, alisema jengo hilo wamelibuni wenyewe litakuwa na mambo kadhaa muhimu ikiwamo mfumo mzuri wa ukusanyaji taka, mfumo wa maji wa uhakika na vifaa vya kisasa vya uunganishaji wa mitandao na runinga ambao siyo lazima kufunga ungo.

# Wakurugenzi wapewa kibano ujenzi shule za sekondari wasichana mikoa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa, amewaweka kikaangoni wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuhusu kusuasua kwa ujenzi wa miundombinu ya shule mpya za sekondari katika maeneo yao.

Kutokana na hali hiyo, Mchengerwa ametoa mwezi mmoja kwa wakurugenzi hao kukamilisha ujenzi huo wa shule za bweni za wasichana za mikoa ambazo zimejengwa katika halmashauri zao ili wanafunzi walioripoti katika shule hizo wapate mazingira bora na rafiki ya kupata elimu.

Mchengerwa alitoa maagizo hayo jana wakati akipokea taarifa za ujenzi wa shule 26 za sekondari za wasichana za mikoa wakati wa kikao cha tathmini ya ujenzi wa shule hizo kilichofanyika katika ukumbi wa Arnautoglu, Dar es Salaam.

Waziri Mchengerwa alisema alitegemea wakurugenzi watoe taarifa ya kukamilika kwa ujenzi wa shule hizo kwa asilimia 100 jambo ambalo halijatekelezeka, wakati akiwa kwenye ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Rukwa, alimwahidi kuwa ndani ya mwezi mmoja miundombinu ya shule zote 26 itakuwa imekamilika.

Alisema katika kuhakikisha kazi hiyo inakamilika ndani ya mwezi mmoja, amewapa baadhi ya wakurugenzi wiki mbili, wengine tatu na wengine mwezi mmoja na ukifika wakati huo kusiwe na shule hata moja iliyosalia ujenzi wake.

Hata hivyo, Mchengerwa alisema mkurugenzi anayesimamia shule ya mkoa wa Rukwa, amepewa miezi miwili.

"Hakutakuwa na nyongeza ya muda katika kipindi ambacho tumekubaliana mkamilishe ujenzi wa miundombinu ya shule hizo na sitosita kumchukulia hatua mkurugenzi yeyote atakayeshindwa kukamilisha ujenzi kwa mujibu wa makubaliano yetu," alisisitiza.

Mchengerwa aliongeza kuwa yeye na Rais Samia wanawategemea wakurugenzi hao katika usimamizi wa miradi mbalimbali inayolenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Kagurumjuli Titus, alisema wamepokea maelekezo ya Waziri na kuahidi kuwa manispaa yake itakamilisha ujenzi huo ndani ya siku 15.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Mariam Chaurembo, alisema halmashauri yake kwa niaba ya Mkoa wa Songwe imejipanga kutekeleza maelekezo na Waziri Mchengerwa ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu hiyo ndani ya mwezi mmoja kama alivyoelekeza.

Kikao hicho cha tathmini ya ujenzi wa shule 26 za sekondari za wasichana za mikoa, kilihudhuriwa na wakurugenzi wa halmashauri, maofisa elimu wa sekondari, wahandisi wa halmashauri na maofisa ununuzi wa halmashauri.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa tatu kulia), akikata utepe kuzindua tawi jipya la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) jijini Mbeya juzi. Wengine ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma (wa nne kulia), Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mwanaasha Khamis Juma (wa nne kushoto), Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya hiyo, Arafat Haji (wa tatu kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki hiyo, Joseph Meza (kulia) na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahueni yaja makali uhaba wa mbolea

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetiliana saini mkataba wa makubaliano na kampuni ya Kundi la Kampuni za ESSA kutoka Indonesia kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha mbolea ya Urea mkoani Mtwara.

Ujenzi wa kiwanda hicho ambacho kitakuwa kikubwa na cha aina yake, utachochea ukuaji wa viwanda vya bidhaa hiyo na kukidhi mahitaji ya ndani.

Mradi huo wa miaka mitano una thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.3 (sawa na Sh. trilioni 3.5) utakuwa na ushirikiano wa karibu na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ambalo litasambaza gesi asilia kwenye kiwanda hicho.

Makubaliano hayo yaliingiwa jana jijini Dar es Salaam kati ya TPDC, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na Kundi la Kampuni la PT ESSA Industries Indonesia Tbk (ESSA).

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, alisema ujenzi wa kiwanda hicho ni matokeo ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Indonesia hivi karibuni, ambayo pamoja na mambo mengine alihamasisha wawekezaji kuwekeza Tanzania.

Prof. Mkumbo alisema mradi huo uliotiwa saini ni mkubwa na utaleta mapinduzi katika sekta ya kilimo na kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Waziri Mkumbo alisema kwa sasa Tanzania inaagiza mbolea kutoka nje kwa asilimia 90, hivyo kuanzishwa kwa kiwanda hicho kutapunguza kwa kiasi kikubwa uagizaji wa mbolea kutoka nje.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokuwa katika mkutano wa kimataifa nchini Russia mapema mwaka huu, mahitaji ya mbolea kwa mwaka ni tani 850,000 hivyo kutokana na takwimu za uzalishaji ambazo ni asilimia 10 tu, kiasi kinachozalishwa nchini ni tani 85,000 na tani 765,000 zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Prof Mkumbo alisema mradi huo umekuja muda mwafaka ambao serikali inawekeza juhudi za kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Alibainisha kuwa mpango mkakati wa kilimo kwa miaka 10 ijayo ni nchi kujitosheleza kwa uzalishaji na usambazaji wa mbolea ili kuchochea uzalishaji mashambani na usambazaji wa malighafi viwandani.

Kamishna na Mjumbe wa Bodi ya ESSA, Rahul Puri, alisema mradi huo utazalisha ajira za moja kwa moja 5,000 na zile zisizo za moja kwa moja zaidi ya 300,000.

Puri alisema huo ni mpango mzuri wa kuongeza thamani ya maliasili za nchi na kuongeza ukuaji wa kilimo na kuboresha maisha.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Francis Mwankapalila, alisema mahitaji ya awali ya gesi asilia katika kiwanda kipya cha mbolea yatakuwa futi za ujazo milioni 70, jambo ambalo shirika litahakikisha upatikanaji wa kutosha ili kurahisisha uendeshaji wa kiwanda hicho.

Mwankapalila alisema wataanza kusambaza gesi mwaka 2027 kwa miaka 20 wakisambaza kati ya futi za ujazo milioni 70 hadi 100 kiwandani hapo.

Takwimu zinaonyesha kuwa hifadhi ya gesi asilia nchini inakadiriwa kufikia futi za ujazo trilioni 54.57 ikiwa na uzalishaji wa futi za ujazo bilioni 110 kwa mwaka kutoka maeneo matatu ya Songo Songo, Mnazi Bay na Kiliwani Kaskazini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Terry, alisema kituo kitaendelea kuvutia uwekezaji zaidi wa kimkakati katika sekta mbalimbali ili kuchochea maendeleo, huku akiihakikishia ushirikiano ESSA Group.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, aliahidi kuwa wataendelea kuvutia uwekezaji katika sekta hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ugawaji vizimba vya biashara uangaliwe kuepusha malalamiko

**JIJI** la Dar es Salaam sasa linavutia katika baadhi ya masoko ambayo yamemalizika ujenzi na kuleta sura mpya.

Masoko mengi yanayojengwa hivi sasa ni ya ghorofa ambayo hayachukui eneo kubwa la kiwanja na pia kutoa nafasi ya kupata vyumba vingi vya kufanyia biashara hizo.

Kabla majengo hayo ya kisasa hayajajengwa kulikuwa na masoko yaliyojengwa kienyeji ambayo hata miundombinu yake haikuwa rafiki kwa wateja.

Masoko mengi hasa wakati wa mvua yanageuka kuwa kero kutokana na njia za kuingia kwenye masoko hayo kujaa matope na maji machafu.

Pia wafanyabiashara wengi walikuwa hawana maeneo maalumu ya kuuza bidhaa zao hasa wale wadogo na kuishia kuzipanga chini.

Lakini kwa utaratibu huu wa kujenga masoko ya kisasa umesaidia kuwa na nafasi nyingi zinazoweza kuwachukua wafanyabiashara wengi.

Hata hivyo, baada ya masoko hayo kukamilika kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara waliokuwa kwenye masoko hayo toka mwanzo kutopewa kipaumbele kama walivyoahidiwa wakati ujenzi wa majengo mapya ulivyoanza.

Malalamiko yanatokana na wafanyabiashara hao kudai kuwa kuna baadhi ya watu hawakuwapo kwenye soko hilo, lakini sasa wanaonekana na ndio wanaopewa kipaumbele.

Uzoefu wa malalamiko umeanza tangu soko jipya ya Machinga Complex, Ilala Mchikichini, ambapo wafanyabiashara wadogo walilalamika baadhi yao kukosa vizimba, au kupangiwa vya juu ambako wateja wengi hawafiki.

Kituo cha biashara cha Mwenge pia kumekuwa na malalamiko kuwa wafanyabiashara waliokuwapo tangu mwanzo katika eneo hilo ambao waliahidiwa kupewa kipaumbele cha kupewa nafasi, waligeukwa na badala yake wenye uwezo kifedha kupewa kipaumbele.

Hali kama hiyo ilijitokeza katika soko jipya la Kariakoo, ambalo liliungua moto na kujengwa upya, huku wafanyabiashara waliokuwa wakifanya shughuli zao hapo, kuahidiwa kuwa wao ndio watakaopewa kipaumbele soko litakapokamilika.

Hata hivyo, malalamiko yale yale yaliyojitokeza katika masoko mengine ndio yanayojitokeza katika soko hilo na kusababisha sintofahamu.

Tatizo kama hilo limejitokeza tena katika soko la Tandale, ambako kumezuka vurugu baada ya wafanyabiashara kulalamika kubadilishiwa maeneo ya kufanyia biashara na viongozi wa soko na Halmashauri ya Manispaa Kinondoni.

Wafanyabiashara hao wameshutumu viongozi wao kwa madai ya kuingiza watu wapya wasio wafahamu.

Sintofahamu hizi zinaweza kusababisha vurugu ambazo zingeweza kuzuilika kama ungewekwa utaratibu mzuri na unaofuatwa.

Kama wafanyabiashara hao waliahidiwa kupewa kipaumbele cha kupata maeneo, iweje baada ya soko kukamilika, utaratibu ukiukwe?


Madai ya wafanyabiashara hao ni kuonekana hawana thamani kuwapo kwenye soko hilo baada ya soko kuwa la kisasa na wanaostahili kufanya biashara ni wenye mwonekano unaofanana na soko hilo.

Ni vizuri viongozi wa soko na manispaa wakakaa pamoja na wafanyabiashara hao kuwaelewesha utaratibu badala ya kupewa lawama ambazo si za kweli.

Kila jambo linahitaji elimu ili watu waelewe kuepusha migongano na sintofahamu ambazo mwishowe husababisha vurugu.

Wafanyabiashara wasikilizwe maoni yao na viongozi watoe majibu ili kupata mwafaka na biashara iendelee kwa faida ya taifa na wananchi wenyewe kuimarisha uchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wasafirishaji isikieni DCEA

**MATUMIZI** ya dawa za kulevya, yanatajwa na wataalamu wa afya ya ubongo na uti wa mgongo kuwa ni kisababishi cha msongo wa mawazo na magonjwa ya akili.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, kutumia dawa hizo, kunaathiri zaidi sehemu za ubongo zilizo karibu na sikio, na kwamba hapo kuna sehemu ya ndani zaidi inayohusika na kazi mbalimbali kama kuhifadhi kumbukumbu za muda mfupi za matukio mbalimbali.

Wabobezi wa afya wanafafanua kuwa, sehemu hiyo pia inafanya kazi ya utambuzi wa hisia ikiwamo furaha au huzuni na kwamba kutumia dawa kunaingilia mfumo huo na kusababisha ushindwe kufanya kazi kwa namna inavyotakiwa.

Inaelezwa kuwa, kutumia dawa hizo kunapokithiri na mtumiaji anapofikia katika hali hiyo, mwathirika anaweza kujikuta anakumbana na tatizo la afya ya akili na kwamba, madhara ya dawa hizo ndiyo yanayosababisha zipigwe marufuku duniani kote.

Maelezo hayo ya wataalamu wa afya, yanaonyesha wazi kwamba kuna umuhimu wa kuwa makini na kuwaelimisha na kuwalinda vijana ili waepuke kuingia katika matumizi ya dawa hizo hatari kwa afya.

Ripoti ya Dunia ya Dawa za Kulevya mwaka 2023 iliyozinduliwa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), inaonyesha kuwa zaidi ya watu milioni 296 duniani wanatumia dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, vijana ndio walio hatarini zaidi kutumia dawa za kulevya na kuathirika zaidi na ugonjwa wa matumizi ya dawa hizo duniani huku Afrika ikiwa na asilimia 70 ya watu wanaopata matibabu dhidi ya dawa hizo wengi wakiwa chini ya umri wa miaka 35.

Kwa Tanzania, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) inaendelea kuwasaka wanaofanya biashara ya dawa hizo, katika maeneo mbalimbali ili kulinda afya za Watanzania.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, anasema Aprili 4 mwaka huu, mamlaka hiyo ilikamata kilo 767.2 za dawa za kulevya katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga.

Lyimo katika ufafanuzi wake, anataja aina ya dawa zilizokamatwa zilikuwa ni pamoja na heroine kilo 233.2, methamphetamine au 'metha' kilo 525.67 na skanka kilo 8.33, huku watu 21 nao wakikamatwa.

Wakati huu ambao mamlaka hiyo inaendelea na msako, inatoa tahadhari kwa madereva wa mabasi na makondakta kuwa wawe makini, kwa kuwa mabasi hayo yamekuwa yakitumika kusafirisha dawa hizo.

Mamlaka hiyo inasema imebaini kuwa, kwa sasa mabasi yanatumika kama njia ya kurahisisha usafirishaji wa dawa hizo kwenda maeneo mbalimbali nchini na kwamba madereva na makondakta wawe makini.

"Ninawatadharisha madereva wa mabasi kwamba wawe makini, tukikuta basi linasafirisha dawa hizo, tutawakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria," ndivyo anavyosema Kamanda Lyimo.

Huo unaweza kuwa mtihani kwao, kwa sababu sio wataalamu wa kutambua dawa hizo, ninadhani ni vyema mamlaka hiyo ikawapa elimu ili iwe rahisi kutambua dawa hizo na kutoa taarifa.

Kwa nini? Kwa sasa mamlaka hiyo inasema imebaini mbinu mpya ya ufichaji wa dawa za kulevya inayotumiwa kuzificha kwa ustadi katika vifungashio vilivyoandikwa majina ya kahawa au chai.

Hivyo, kwa mbinu hizo, madereva na makondakta wanaweza kujikuta katika mtihani mkubwa iwapo DCEA itaamua kukomaa nao katika ukaguzi wa dawa hizo katika mabasi.

Kwa mbinu hiyo ya DCEA, makondakta na madereva wawahusishe wataalamu wa dawa za kulevya kupima vifurushi hivyo kabla ya kukabidhiwa kwao ili kuvisafirisha.

## Babalishe, mamalishe waitwa mifuko ya pamoja na mitaji

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imehamasisha wafanyabiashara wadogo, wakiwamo mamalishe na babalishe kuwekeza katika mifuko ya pamoja na mitaji ili kunufaika na fursa zinazopatikana katika sekta ya fedha hususani masoko hayo.

Rai hiyo ilitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Utafiti na Uendelezaji Masoko wa CMSA, Afred Mkombo wakati akitambulisha rasmi mkataba wa kuendesha mfuko wa uwekezaji wa pamoja kutoka kampuni ya Zan Securities wa Timiza Fund.

Alisema ni vyema wafanyabiashara wadogo wakatumia fursa hiyo kuwekeza ili kujiongezea kipato na kuinua uchumi wao kwa sababu haihitaji fedha nyingi.

"Na kupitia mfuko huu wa Timiza Fund ambao uko mahsusi kwa ajili ya vijana, wanawake, makundi maalum, taasisi na mifuko ya hifadhi ya jamii, wanaweza kuwekeza hata kuanzia Sh. 10,000 na lengo lake ni kuunga mkono jitihada za serikali katika kuongeza wigo wa upatikanaji huduma za fedha kwa wananchi wengi mijini na vijijini.

"Mara nyingi tumezoea kwamba kuwekeza ni mpaka uwe na fedha nyingi sana, ni vyema tukabadilika, watu wafahamu kwamba fedha yoyote ya ziada mtu anaweza kuiwekeza ili baadaye ajiongezee kipato, hata ukiwa machinga, mamalishe au mwingine yeyote anaweza kuwekeza," alisema.

Ofisa huyo alisema mifuko ya uwekezaji wa pamoja mpaka sasa iko 10 na kwamba kwa sasa kuna mwamko mkubwa wa uwekezaji kwa wafanyabiashara wadogo.

"Japokuwa katika eneo hili halijafanya vizuri kama ilivyo kwa nchi za jirani, hivi karibuni tumeona mwamko wa makundi mbalimbali kujitokeza kuwekeza ikiwamo wafanyabiashara wadogo.

"Kwahiyo, tunaendelea kuwatia moyo kwamba wasiache kufanya hivyo kwa kuwa hiyo itawasaidia kujiongezea kipato na kuinua uchumi wao," alisema Mkombo.

Mkurugenzi Mkuu wa Zan Securities, Alfred Masumbuko, alisema vipande vya uwekezaji vya mfuko wa Timiza vinaweza kutumika kama dhamana kwa mwekezaji wa mfuko huo kupata mkopo kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

"Hii pia ni fursa kwa vijana wadogo kuanza kuwekeza, chochote anachokipata anaweza kufanya hivyo na akajikuta amejiongezea kipato," alisema Masumbuko.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa tatu kulia), akipata taarifa fupi kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Mawasiliano na Mahusiano ya Umma wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu (wa pili (kushoto), kuhusu jitihada mbalimbali zinazofanywa na benki hiyo katika sekta ya afya, wakati wa kongamano la Afya Kitaifa, lililoandaliwa na Taasisi ya Benjamin Mkapa (BMF), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kulia) na (katikati) ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa BMF, Dk. Ellen Senkoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TFS yaonya ukataji mikoko

**Na Halfani Chusi**

OFISA Uhifadhi kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, Mwanahawa Matimbwa amekemea baadhi ya wanakijiji wanaokata mikoko kwa ajili ya shughuli za kibinadamu.

Alitoa onyo hilo juzi wilayani humo wakati wa kusherehekea Siku ya Mikoko Duniani iliyofanyika Kijiji cha Mdimni.

Katika maadhimisho hayo, Mwanahawa alisema mikoko ina faida nyingi ikiwamo kupambana na mabadiliko ya tabianchi, mawimbi makali baharini, kusaidia katika ustawi wa samaki na viumbe baharini.

"Mikoko ina faida nyingi sana, tunachokifanya kwa sasa tunaendelea kutoa elimu katika vijiji vinavyozungukwa na hifadhi za mikoko, ili viweze kutambua na kujua umuhimu wake.

"Katika kulinda pia tunafanya doria mara kwa mara, mara moja kwa wiki na wakati mwingine mara bili kwa wiki tukishirikiana na wananchi wa vijiji husika.

Kiongozi wa Miradi ya Uhifadhi wa Mikoko katika vijiji vya Mdimni, Nganje na Kifumangao, Ramadhani Mkayi alisema lengo la maadhimisho hayo kufanyika kijijini huko ni kuamsha hamasa ya utunzaji mikoko kwa wananchi wanaozungukwa nayo.

Pia alisema katika sherehe hiyo walipanda miti 600 ya mikoko pamoja na kutoa elimu ya namna ya kuhifadhi kwa wanakijiji, ili waweze kujua umuhimu wake na kuitunza.

Alitaja hasara za kukata mikoko kwamba ni kuharibu mazalia ya samaki na makazi ya viumbe wengine wengi.

"Nizishukuru taasisi zisizokuwa za kiserikali; TCCI na Mazingira Plus zinazojihusisha na uhifadhi wa mazingira na kutoa suluhisho la mabadiliko ya tabianchi kwa kuhakikisha maadhimisho haya yamefanyika. "Tunashukuru uongozi wa Wilaya ya Mkuranga kwa kutupatia ushirikiano wa kutosha, lakini pia taasisi ya The Oceans, Assemble Insurance kwa kutuunga mkono katika tukio hili," alisema.

> **Katika maadhimisho hayo, Mwanahawa alisema mikoko ina faida nyingi ikiwamo kupambana na mabadiliko ya tabianchi, mawimbi makali baharini, kusaidia katika ustawi wa samaki na viumbe baharini.**

Ofisa Mtendaji wa Mdimni ambako maadhimisho hayo yalifanyika, Idd Mwagala aliishukuru taasisi hizo kuadhimisha siku hiyo katika kijiji chake, akisisitiza imesaidia wananchi wake kupata uwelewa mkubwa katika utunzaji mikoko.

Alisema awali walikuwa wanakata mikoko na kutumia kujenga nyumba zao; baada ya kupewa elimu wanaitunza.

Mwanakijiji wa Mdimni, Maria Hasan alishauri serikali iwapatie elimu ya utunzaji hifadhi za mikoko, ili wote wanaoishi karibu waweze kujua faida yake.

Mwanakijiji mwingine Maimuna Mkoko aliomba serikali iwawezeshe kupata mikopo ili waweze kujishughulisha na kilimo cha umwagiliaji.

"Tunaomba TFS ituwezeshe sisi watunzaji mikoko, kila siku tunaamka asubuhi tunakwenda kulinda na kupanda mingine, lakini hatupati chochote. Tunaomba serikali itukumbuke maana huku kijijini hali ni ngumu," alilalama mwanakijiji huyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Bandari ya uvuvi kuajiri watu 30,000

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema mradi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko, unaokaribia kukamilika unatarajia kutoa ajira kwa zaidi ya watu 30,000.

Aidha, amewataka wakazi wa Kilwa kuitunza bandari hiyo ili kuwa na manufaa ya muda mrefu.

Waziri Ulega aliyasema hayo jana alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo unaofanyika wilayani Kilwa, mkoani Lindi.

Alisema, hadi sasa mradi huo umeshatoa ajira kwa vijana 570 na kuwa utakapo kamilika utatoa ajira elfu 30 katika nyanja mbalimbali ikiwamo uvuvi na uchuuzi wa samaki.

Aidha, aliwasihi wananchi hao kutunza mradi huo ili baadaye uinue uchumi wao kupitia biashara ya samaki, kwani kukamilika kwake kutachochea maendeleo ya mtu mmoja na taifa.

"Mradi huu tuutazame kama mboni ya jicho letu ili uwe endelevu kwa maana ukikamilika utainua uchumi wa Kilwa, ukanda wa Kusini na Taifa kwa ujumla.

"Leo nimekuja kutembelea mradi huu nimewakuta vijana wanafurahia kazi wanayoifanya. Vijana wa taifa zima watapata fursa ya kufanya. Tunatarajia vijana wasiopungua 30,000 kutoka maeneo mbalimbali watapata ajira hapa," alisema.

Alisema ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko na mpaka sasa umefikia asilimia 63 na unatarajiwa kukamilika Februari, mwakani na kuwasisitiza wanaousimamia kuhakikisha unamalizika kwa wakati, ili Watanzania waanze kunufaika mapema.

Pia alisema bandari hiyo inayojengwa kwa fedha za ndani ni mradi wa kielelezo unaotekelezwa chini ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (wa tatu kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa watu walioshiriki uzinduzi wa sera ya taifa ya biashara jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Teknolojia ya 5G yazidi kusambaa

Na Mwandishi Wetu

RIPOTI ya hali ya mawasiliano ya robo mwaka Aprili hadi Juni mwaka huu, imeonesha kuwa teknolojia ya mawasiliano ya uzao wa tano (5G) imeenea nchini kwa asilimia 15.

Ripoti hiyo iliyotolewa hivi karibuni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeonesha kuwa, teknolojia hiyo imewezesha upatikanaji na matumizi ya intanet ya kasi kubwa yenye ubora wa juu nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema teknolojia hiyo iliyoingia Tanzania Agosti 2022, inapatikana katika eneo la asilimia mbili ya eneo la Tanzania ikilinganishwa na kiwango cha asilimia moja kilichofikiwa Machi, mwaka huu.

"Vifaa vimefungwa kwenye minara 754 ya mawasiliano ya simu za mkononi nchini kote. Miundombinu hii inahakikishia watumiaji wa intaneti yenye ubora wa juu na kasi kubwa, huduma ambayo ni mhimili mkubwa wa uchumi wa kidijitali unaojengwa Tanzania," alisema.

Alisema mawasiliano ya simu za mkononi yameendelea kutoka uzao wa kwanza wa analojia, uliowezesha maongezi tu, hadi uzao huo wa tano (5G).

"Uzao wa pili (2G) unawezesha maongezi na ujumbe mfupi, wa tatu (3G) unawezesha vyote hivi, huduma za intaneti na data. Uzao wa nne (4G) una sifa za uzao wa tatu na unawahakikishia watumiaji wake intaneti ya kasi. Pamoja na minara ya 5G, kulikuwa na 11,777 ya 4G, mingine 12,366 ya 3G na 13,470 ya 2G Juni 2024," alisema.

Kuhusu kuenea na kupatikana kwa huduma za teknolojia hiyo kati ya Machi na Juni mwaka huu, mkoani Dar es salaam, Dk. Bakari alisema huduma za 3G zilifikia asilimia 89 ya watu Tanzania Juni, kutoka asilimia 88 Machi 2024.

"Kijiografia zimeenea asilimia 73 ya Tanzania kulinganisha na asilimia 72 Machi. Mawasiliano ya 4G yameenea kwa asilimia 83 ya watu kutoka asilimia 80 na kijiografia yanafika asilimia 69 ya eneo la Tanzania, kutoka asilimia 64,"alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Bakari, minara ya 5G, kulikuwa na 11,777 ya 2G, mingine 12,366 ya 3G na 13,470 ya 2G Juni 2024.

"Matumizi ya intaneti yameongezeka kwa asilimia saba kati ya Aprili na Machi 2024. Laini za simu na vifaa mbalimbali vinavyotumika kupata huduma za intaneti vimeongezeka kutoka milioni 36.8 Machi 2024 hadi milioni 39.3 Juni," alisema. Alisema kipimo cha kuenea huduma za intaneti ni laini za simu, simu za mezani na uunganishwaji wake kwenye mifumo ya simu na kutumika kupata huduma hizo ndani ya miezi mitatu.

Dk. Bakari alifafanua kuwa watumiaji wengi wanapata huduma za intaneti kuitia simu zenye uwezo mkubwa, au simu janja, vishkwambi, kompyuta na modemu.

Aidha, amesema simu janja zimeenea miongoni mwa watu Tanzania kwa asilimia 31.6, kutoka asimilia 31.5 Machi mwaka huu zilienea kwa asilimia 25 Desemba 2022.

Dk. Bakari alisema mapema mwaka huu kuwa taasisi yake itafuatilia kwa kina gharama za simu janja, kwa kuwa kuenea kwake na kupatikana kwa watumiaji wengi kutaharakisha kufikiwa lengo la asilimia 80 ya Watanzania kuwa wanatumia huduma za intaneti ifikapo Desemba 2025.

"Kasi ya kupakua na kupakia data kwenye intaneti imeongeze kwa wastani wa megabaiti 11.4 kwa sekunde hadi megabaiti 12 kwa sekunde kati ya Aprili na Juni,"alisema.

Aidha, alisema takwimu hizo zinaonesha kuwa; taasisi, makampuni na watu binafsi wanaotumia kikoa cha Tanzania, yaani 'dot tz' wameongezeka kutoka 29,968 Machi 2024 hadi 30,698 Juni mwaka huu.

Kikoa cha dot tz ni utambulisho rasmi wa Tanzania kwenye mtandao wa intaneti, kama ulivyo msimbo wa +255 kwa mawasiliano ya simu.

## Tisa mbaroni madai kutorosha dhahabu

Na Shaban Njia, KAHAMA

WATU tisa wamekamatwa na Ofisi ya Madini, Mkoa wa Kimadini wa Kahama kwa kushirikiana na Kikosi Maalum cha Kudhibiti na Kupambana na Utoroshaji Madini mkoani Shinyanga, dhahabu yenye thamani ya Sh. milioni 8.6 na fedha taslimu Sh. milioni 3.57.

Vigogo hao ni wafadhili wa utoroshaji madini, wanunuzi pamoja na ofisa madini anayesimamia masoko, ambao walikutwa na gramu 45.35 za dhahabu.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Winfrida Mrema, akizungumza na waandishi wa habari alisema watu hao walikamatwa kufuatia ukaguzi wa siku mbili walioufanya katika Mgodi wa Mwime Kata ya Zongomela Manispaa ya Kahama kuanzia Julai 24 hadi 25, mwaka huu.

Alisema katika ukaguzi wao walioufanya baada ya kutoa elimu kwa wachimbaji walifanikiwa kuwakamata watu tisa, kati yake wanne walikuwa wafadhili wa ununuzi wa madini, wanne wanunuzi na mmoja ni ofisa madini aliyekuwa akifanya kazi kwa mkataba.

Alisema ofisa huyo tayari wamesitisha mkataba wake na kumwondoa kazini kwa kuisababishia serikali kukosa mapato yake, vilevile ameachiwa baada ya kuhojiwa.

Mrema alisema ofisa madini huyo alikuwa akishirikiana na wanunuzi katika kupunguza thamani ya dhahabu wakati wa soko na kuisababishia serikali kukosa mapato yake, na wamelazimika kufuta leseni kubwa ya biashara namba DL003/KHM/2023-2024 yenye jina la Gold Trade Company ambapo mmiliki wake ni miongoni mwa wafadhili hao.

Hata hivyo, alisema kwenye operesheni hiyo waliongeza uzalishaji wa dhahabu kutoka kilogramu 5.1 kwa mwezi Juni mpaka kilogramu 6.4 kwa mwezi Julai sawa na ongezeko la kilogramu 1.3 na kuwa operesheni hiyo itakuwa endelevu katika migodi midogo mingine ili kudhibiti ununuzi wa madini kwa njia isiyo halali.

"Tuliowakamata walikuwa wakinunua dhahabu kwenye mialo kinyume na sheria kwa kutumia mizani ambayo haijahakikiwa na mamkala ya vipimo, kwani dhahabu inatakiwa kununuliwa sokoni na sio vinginevyo," alisema Mrema.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kukamatwa kwa watu hao kupitia kikosi kazi maalumu cha kudhibiti na kupambana na utoroshaji wa madini.

Alisema kwa sasa majina yao yamehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi na kuwa baada ya kikosi hicho kukamilisha uchunguzi wake taarifa rasmi itatolewa.



## Uamuzi kesi kada wa CHADEMA dhidi ya IGP, wengine Agosti mosi

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Tanga, inatarajia kutoa uamuzi wake Agosti mosi mwaka huu, kuhusu hoja zinazobishaniwa katika shauri la maombi madogo ya jinai, lililofunguliwa na Kombo Mbwana, dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) na wenzake.

Jaji Happyness Ndesamburo, anayesikiliza shauri hilo lililofunguliwa kwa hati ya dharura, amepanga kutoa uamuzi huo Alhamisi wiki hii, huku hatima ya Kombo iwapo atapata dhamana au laa, ikitarajiwa pia kujulikana siku hiyo.

Aidha, uamuzi huo utatoa picha halisi kama kesi aliyoifungua mahakamani kuhusu IGP na wenzake inastahili kuendelea kuwapo mahakamani kama kesi halali.

Kombo amefungua kesi hiyo dhidi ya IGP, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga (RPC), Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Kesi hiyo ilifunguliwa Julai 17 mwaka huu na mawakili tisa, akiwamo Paul Kisabo kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Peter Madeleka na mawakili wengine saba wanaomtetea Kombo.

Katika kesi hiyo, Kombo anaiomba mahakama ilazimishe mamlaka husika au wanaomshikilia kwa muda mrefu kumfikisha mahakamani na kueleza mashtaka yanayomkabili.

Pia anaiomba mahakama iamuru aachiwe huru na kulipwa fidia kwa kushikiliwa kinyume cha sheria, kwa takribani siku 29.

# Prof. Mkenda ataka uzalishaji wataalamu wengi nishati jadidifu

**Na Cynthia Mwilolezi,** HAI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amezindua rasmi mradi wa ujenzi wa Ndaki ya Kikuletwa ya Chuo cha Ufundi Arusha, ambao ni moja ya miradi minne mikubwa inayotekelezwa na serikali kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 187.

Katika mradi huo, nchi tatu ikiwamo Tanzania, Kenya na Ethiopia zitanufaika kwa kuzalisha wataalamu wa nishati jadidifu.

Jana Waziri Mkenda, aliweka jiwe la msingi katika Ndaki ya Kikuletwa iliyoko Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Prof. Mkenda alisema chuo hicho kitasaidia kuzalisha wataalamu wa nishati jadidifu ambao watasaidia wananchi kutunza mazingira kwa kuepuka kutumia nishati za kuni na mkaa.

"Nishati jadilifu ni muhimu katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia na jua la kutosha tunalo, upepo na maji, hivyo kuzalishwa kwa wataalamu wa eneo hili itatusaidia sana kama nchi,"alisema.

Aidha, alishukuru serikali kutoa fedha nyingi katika sekta ya elimu, ambapo katika mradi huo wa nishati jadilifu katika eneo la Kikuletwa wametoa Sh. bilioni 37.5 hadi kukamilika kwake .

"Huu ni mradi mmojawapo kati ya miradi minne itakayogharimu zaidi ya Sh.bilioni 187.5 inayotekelezwa na serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia (WB) ukishirikisha nchi tatu Kenya, Tanzania na Shirikisho la Jamhuri ya Ethiopia.

"Ambapo katika nchi hizi tatu jumla ya miradi 16 inatekelezwa ambapo kwa Tanzania tunatekeleza minne, ikiwamo huu wa nishati jadilifu uliopo Kikuletwa," alisema.

Pia ameagiza vyuo vya ufundi nchini kujenga uhusiano mzuri na kampuni kubwa ya utengenezaji magari ya nje ya nchi, ili kusaidia vijana wanaosomea ufundi nchini, kuweza kutengeneza magari ya kisasa yanayokuja nchini pindi yanapoharibika.

"Hivi sasa tuna tatizo kubwa la kupata mafundi wa magari haya ya kisasa tunayonunua sisi serikali na wananchi mmoja mmoja yanapokuja nchini pindi yanapoharibika mengi tunakosa mafundi wa kuyatengeneza hivyo tujenge mahusiano mazuri na makampuni ya magari huko nje tusijifungie milango ukiwezekana waje kwetu nasi wanafunzi wetu waende huko kujifunza," alisema.

Kadhalika, aliagiza nguvu kazi ielekezwe zaidi katika rasilimali ya nguvu kazi ya watu, ikiwemo kujenga mabweni yatakayoendana na uwiano wa wanafunzi watakaokuja kusoma chuoni hapo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Caroline Nombo, alisema mbali na ujenzi wa kituo cha Kikuletwa, miradi mingine ni wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) unaotekelezwa na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Teknolojia ya Ngozi ya Mwanza na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Awali, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi Arusha, Francis Kisangire, alisema kampasi hiyo, imekamilika kwa hatua ya kwanza (phase one) ingawa bado inaendelea kujengwa na alishukuru serikali kuhakikisha wataalamu wabobezi wanazalishwa kupitia kampasi hiyo.

Mkuu wa Chuo cha ATC, Prof. Mussa Chacha alisema uwepo wa chuo hicho kinaongeza umahiri na udahili zaidi katika kuzalisha wataalamu wabobezi wa masuala mbalimbali ya ufundi, utoaji wabobezi wa aina mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho cha ufundi.




Mbunge wa Jimbo la Kiteto, mkoani Manyara, Edward Ole Lekaita (kushoto), akipanda mti kwa ajili ya kutunza mazingira katika viwanja vya Shule ya Sekondari Kibaya, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waziri awapa mbinu wanawake kukwepa mikopo umiza mtaani

**Na Mary Mosha,** SAME

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, amewataka wanawake kuacha kuchukua mikopo umiza mtaani na badala yake wachukue ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri zilizoainishwa nchini.

Aidha, amesema baadhi ya wanawake wamefikia hatua ya kuzikimbia familia zao kutokana na kero wanazozipata kutoka taasisi za kukopesha fedha ambazo zimewapa mikopo umiza.

Naibu Waziri huyo alitoa ushauri huo jana katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, alipokwenda kuzungumza na viongozi wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), Tarafa ya Mamba Vunta, Gonja na Ndungu.

"Ndoa zetu zimekuwa zikivunjika, lakini tumekuwa tukikimbia familia. Sasa serikali imerejesha mikopo ya asilimia 10, hivyo tuachane na mikopo umiza tuchukue hii ya serikali tujinufaishe.

"Wanawake tumekuwa tukiumizwa sana na hii mikopo umiza, ambayo ni kausha damu. Ndoa zetu zimekuwa zikivunjika lakini tumekuwa tukikimbia familia sasa serikali imerejesha mikopo; hivyo tuachane na mikopo umiza tuchukue hii ya serikali tujinufaishe."

"Serikali ilitangaza kurejesha mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalum kuanzia Julai mosi mwaka huu."

Aprili 16, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, wakati akiwasilisha bungeni Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2024/25, alisema halmashauri 10 za majaribio zitaanza utoaji wa mikopo hiyo kwa kutumia benki.

Mikopo inayotarajiwa kutolewa ni Sh. bilioni 227.96, ambapo Sh. bilioni 63.67 ni fedha za marejesho zilizokuwa zikiendelea kukusanywa kutokana na mikopo iliyokuwa iliyotolewa kabla ya kusimamishwa.

Alisema Sh. bilioni 63.24, ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na Sh. bilioni 101.05 ambazo zimetengwa kutokana na makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka 2024/25.



# Meya ataka hatua kali kudhibiti utoro shuleni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MSTAHIKI Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, amelalamikia tatizo la kukithiri kwa utoro wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na kuwataka madiwani kushirikiana na maofisa elimu wa kata na watendaji kudhibiti tatizo hilo.

Kiongozi huyo alisema hayo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, cha robo ya nne ya mwaka 2023/24 kwa ajili ya uwasilishaji wa taarifa za kata.

Alisema katika Manispaa ya Shinyanga kunatatizo kubwa la utoro wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, hali ambayo siyo nzuri kitaaluma.

“Watoto wengi hawaendi shule, sasa niwaombe madiwani twendeni tukasaidizane kufanya jitihada za dhati kumaliza tatizo la utoro kwa wanafunzi na wote wahudhurie shule,”alisema Masumbuko.

Aidha, katika baraza hilo iliibuliwa kero ya uhaba wa watendaji wa vijiji na mitaa, na kuiomba serikali kuajiri watumishi hao ili kurahisisha utendaji kazi na kuwatumikia wananchi kwa ufasaha. Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Manispaa ya Shinyanga, Pius Sayayi, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Alexius Kagunze, alisema kwa mwaka 2024/25 wamepata kibali cha kuajiri watumishi 151 wakiwamo watendaji hao wa vijiji na mitaa.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Godfrey Mnzava (katikati), akikata utepe wakati wa uzinduzi wa klabu ya mazingira ya Shule ya Sekondari Kamunyonge, mjini Musoma mkoani Mara jana. Mnzava aliwataka wanafunzi wa shule hiyo kuwa mabalozi wa mazingira kwenye jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA, TAMWA wataka ubunifu kwenye maudhui

**Na Benny Kingson,** TABORA

WAANDISHI wa Habari nchini wamekumbushwa kuongeza ubunifu katika uandaaji wa maudhui ya habari, kwa kuhakikisha wanaandaa habari zenye kuibua fursa za kiuchumi zitakazoleta tija kwa jamii.

Rai hiyo imetolewa juzi mkoani Tabora na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Nchini (TAMWA) wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari, maofisa habari na mameneja wa vituo vya habari kutoka mikoa ya Tabora na Kigoma.

Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Rodney Mbuya, aliwataka wanahabari kuhakikisha wanachangia kuleta fursa mbalimbali katika sekta zote, ili jamii izitumie kupata maendeleo na haraka sambamba na matumizi ya Akili Mnemba, ili kuokoa muda katika utendaji.

Aidha, Mbuya alizitaka taasisi zote za umma kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa waandishi wa habari, kuwapa taarifa mbalimbali za miradi ya kimkakati na za maendeleo, ili jamii iweze kuzipata katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Tabora, Ramadhani Kapela, alisema kupitia mafunzo hayo ana uhakika waandishi hao watafanya kazi kwa weledi na kuisaidia jamii kuondokana na umaskini.

Aidha, aliahidi kushirikiana na viongozi wa manispaa hiyo kuhakikisha wanasimamia waandishi wa habari wanapata taarifa husika kwa wakati.

Aliwakumbusha baadhi ya waandishi wanatoa taarifa potofu mtandaoni kuacha tabia hiyo mara moja, kwa kwua wanaharibu maadili yao na jamii wanayoishi.

# Kaya 32,000 hazina vyoo bora Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAYA 32,343 kati ya 104,686 sawa na asilimia 30.8 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, zimetajwa kutokuwa na vyoo bora na salama hali inayohatarisha afya za wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Afya wa Halmashauri ya Kahama, Nuru Abel, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya uhifadhi wa mazingira na matumizi sahihi ya choo bora katika manispaa hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo, manispaa imebuni mbinu mpya ya kuhamasisha wananchi kujengwa vyoo bora vyenye maji tiririka kwa kutumia njia ya uchefushaji (CLTS).

Nuru alisema njia hiyo inayolenga kuwahamasisha wananchi wanakuwa na vyoo bora na kuondokana na magonjwa ya mlipuko wamekuwa wakishirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania na kufanikiwa kushawishi kaya 72,343 ambazo mpaka sasa zina vyoo bora.

Aidha, alisema wananchi hayo licha ya kuwa na nyumba bora, wana utamaduni wa kujenga vyoo mbali na makazi yao umbali wa mita 200 hadi 300 ambavyo pia vimejengwa kwa tope na nyasi kwa madai haihitajiki kuwa karibu yao.

Alitaja sifa za choo bora kuwa kinatakiwa kujengwa pande nne, paa, mlango wa kufanga na kufungua, sakafu na miundombinu ya kunawa mikono.

Mkazi wa Kinaga, Sharife Ramadhani alisema hawakujua sifa za choo bora na kuwa anajiandaa kujenga choo bora ili kukabiliana na mlipuko wa magonjwa.

Aidha, alishauri hatua kali kuendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini wanaobainika kutokuwa na choo hali itakayosaidia kuondokana na kujisikia vichakani ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko.

# Waitara awatuliza wanaotaka Mji wa Sirari kuwa mamlaka

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MBUNGE wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, amewaomba wadau na wananchi wanaotamani Mji wa Sirari kuwa mamlaka, kuwa na subra wakati suala hilo linashughulikiwa na serikali.

Waitara alitoa kauli hiyo juzi akizungumza na wajumbe wa halmashauri hiyo mjini Tarime nakueleza kuwa alishapokea majibu ya suala hilo kupitia maswali yake bungeni na kuwataka wajumbe hao kuendelea kuwa na subira.

“Uanzishwaji wa mamlaka yoyote ya eneo la utawala unafuata sheria ikiwa ni pamoja kupitishwa kwanza katika Baraza la Madiwani, unaelekea vikao vya maendeleo wilaya (DCC) hadi Mkoa (RCC), ambapo baadaye uamuzi huo unapelekwa serikali kupitia Wizara ya OR- TAMISEMI,” alisema.

Aidha, alisema zimekuwapo ahadi mbalimbali za madiwani kupandisha hadhi mji huo kutokana na kukidhi vigezo vya utawala, ikiwamo wingi wa watu zaidi ya 25,000 kwa mujibu wa sensa ya 2022, ambako vilevile wajumbe wa Halmashauri ya CCM Wilaya wametajwa kubariki mchakato huo ikiwa ni pamoja na kupitishwa katika Baraza la Madiwani na ngazi za vikao vya wilaya hadi mkoa.

Akiwa Mjini Sirari hivi karibuni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitaja nia ya serikali ni kuleta maendeleo na huduma karibu na wananchi kupitia kutangazwa mamlaka mpya za utawala pale zinapokidhi vigezo.

“Serikali haina pingamizi kuhusu kuanzishwa mamlaka ya mji huu pamoja na maombi kutoka kote nchini iwapo tu maeneo hayo yatakidhi vigezo vinavyotakiwa kisheria hivyo nashauri viongozi waanzishe mchakato huo ngazi za chini kwanza,” alisema Majaliwa.

Baadhi ya wadau wa maendeleo na wanasiasa wilayani hapa

Laurent Nyablangeti walisema wanashindwa kukubaliana na kusubiri utaratibu wa sheria wakidai hiyo ilikuwa ni ahadi ya serikali zaidi ya miaka kumi iliyopita.

Aidha, alidai kuwa ahadi hiyo ilitolewa mwaka 2012 na aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo, Mizengo Pinda lakini mpaka sasa tangazo la mamlaka hiyo halijatoka na kuwa walitarajia tu utekelezaji na siyo kuanza upya ngazi za chini.

# ama

ALHAMISI AGOSTI 1, 2024

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12



DIT yatafiti uchafuzi hewa Dar, kiwango kinatisha dampo Pugu



Ukurasa 14

**Mauaji yanapoweka njia panda afya ya akili na mwili wa mtoto**

# Migodi midogo inavyoendelea kutikisa maambukizi ya VVU na Ukimwi nchini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKOA wa Shinyanga bado unashamiri katika maambukizi ya virusi vya UKIMWI na VVU, ikiwa na asilimia 5.6 juu ya wastani wa kitaifa illiyokuwa nayo awali, asilimia 4.4.

Hiyo ni kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2022/2023, huku vijana wenye umri balehe ndio wahanga wakubwa, kulinganisha na makundi mengine.

Hata hivyo, kasi hiyo ikilinganishwa na mkoa ulikotoka, Shinyanga inaonekana kupungua asilimia 0.3. Matokeo ya utafiti uliopita yalionyesha mkoa ulishamiri asilimia 5.9 mwaka 2017/2018.

Sababu ya mabadiliko hayo, inatajwa kuwa elimu inayotolewa hasa katika matumizi ya kondomu na kufanywa tohara kwa vijana wenye umri miaka 10 na kuendelea.

Chanzo cha ongezeko VVU ni kuwapo ngono zembe hasa kwenye mikusanyiko kama ya minada, magulio, maeneo yanayokuwa na kasi kiuchumi (Senta), migodi midogo ya madini dhahabu, hasa katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa.

Kushamiri maambukizi hayo ya VVU, kumewatia hofu na kuwaibua wachimbaji wadogo migodini hapa, wakieleza namna baadhi yao wanaupata ugonjwa huo kwa kuendekeza 'ngono zembe' wanapopata fedha zitokanakazo na uuzaji mawe ya madini.



Wachimbaji wadogo wa mgodi wa namba tano Mwakitolyo uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wakiosha mchanga unaosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu. **PICHA: SHABAN NJIA**

**WASIMAMIZI WA MIGODI**

Katibu Mkuu wa Mgodi wa Chapakazi and Partners Gold Mine uliopo kijiji cha Wisolele kata ya Segese, Halmashauri ya Wilaya Msalala mkoani Shinyanga, Stephen Lutego, anakiri wachimbaji wako hatarini kupata VVU, kulinganishana makundi mengine kwa sababu ya kuwapo ngono zembe wanazofanya.

Anafafanua kuwa tabia inayochukua nafasi kila kukiuzwa mawe yenye dhahabu, wanufaika wa kuuza dhahabu hujisahau na wanakoswa ushauri sahihi.

Lutego anataja hatua waliyochukua, wameweka utaratibu wa kuzungumza na wachimbaji kabla na baada ya kutoka 'shimoni' kila siku, lengo ni kuwakumbusha walichokifanya katika kutafuta maisha na kuwapatia mifano ya wenzao waliopata VVU na kurejea nyumbani.

Msimamizi wa mgodi wa Mwakitolyo Namba Tano, wilayani Shinyanga, Matemla Michael, anasema wanashirikiana na asasi za kiraia za kudhibiti maradhi hayo, wakiwapatia wachimbaji elimu ya kujikinga na VVU na kwa wanaobainika kuambukizwa, wakubali hatua mpya ya tiba na matumizi ya dawa za kufubaza.

"Wachimbaji wanapata maambukizi bila kufahamu na kwakuwa hatuna desturi ya kupima afya zetu, tunazidi kunyongonyea tu kiafya wanarejea kwenye familia zao wakiwa na hali mbaya", anaongeza.

Anasema hatua ya kukabili hatari hiyo migodini, wameweka boksi za kondomu kwa wahitaji kuondokana na hatari ya ngono zembe zinazofanyika zaidi, baada ya wahusika kulewa pombe.

Michael anawatetea kuwapo wenye maambukizi ya virusii, wanateketeza vyema masharti ya tiba, hata kuwawezesha kufanya kazi kwa ufasaha.

**WACHIMBAJI WADOGO**

Nyundo Samweli, mchimbaji mdogo wa dhahabu mgodi mdogo wa Ntambalale, kijijini Wisolele, kata ya Segese-Msalala anaunga mkono hoja kwamba kinachowaponza kupata VVU, ni starehe zao migodini, baada ya kuuza mawe ya dhahabu, wakisahau mzizi wa maisha yao kwenye familia wanakotoka.

Akiainisha, wanapopata fedha hukimbilia kunywa pombe na kustarehe na wenza wauza miili, waliopanga katika 'nyumba bubu' za kulala wageni na wamekuwa wakiyafanya hayo.

"Mie rafiki yangu alipenda sana starehe kila siku yeye ni mtu wa pombe na wanawake tu, tukipata fedha tunagawana sawa mie najiendeleza kiuchumi kifamilia yeye pombe aliona ni fahari, mwisho wake alipata maambukizi ya VVU akakosa nguvu ya kufanyakazi na amerejea nyumbani kwa familia yake,"

**INAENDELEA UK.13**

MAZINGIRA

# DIT yatafiti uchafuzi hewa Dar, kiwango kinatisha dampo Pugu

## • Usiku hali ni mbaya 'kuliko maelezo'

**Na Christina Mwakangale**

UTAFITI wa ufuatiliaji wa kiwango cha uchafuzi wa hewa katika Jiji la Dar es Salaam uliotumia 'vihisia' (sensor), ulibaini kiwango cha hewa chafu kimekithiri baadhi ya maeneo ya jiji, hasa dampo la Pugu.

Vihisia hivyo vilibaini maeneo mengine ya Dar es Salaam yenye viwanda, kwenye msongamano wa magari na Shule ya Msingi Vingunguti, yamevuka viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Mhadhiri wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Dk. Mbazingwa Mkiramweni, ameiambia Nipashe, hivi karibuni kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), Sabasaba.

"Utafiti huu ulihusisha kufungwa vihisia maeneo tofauti katika Jiji la Dar es Salaam, kufuatilia ubora wa hewa kwa kutumia vihisia 13 vyenye gharama nafuu vya PurpleAir PA-II vilivyotumika kuanzia Mei 2021 hadi Februari 2022.

"Kwa mujibu wa miongozo ya WHO, ubora wa hewa nchini Tanzania unachukuliwa kuwa si salama sana kwa kuwa kiwango cha wastani cha PM2.5 na PM10 (PM-Particular Matter) ni kikubwa kuliko kinachopendekezwa.

"Mradi huu ulikuwa ni wa ushirikiano baina ya Taasisi ya Mazingira ya Stockholm (Stockholm Environmental Institute (SEI) Africa Centre, C40 Climate Leadership Group, DIT pamoja na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (DCC) na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

"Ulibuni na kufunga mfumo wa kufuatilia kiwango cha uchafuzi wa hewa kwa Jiji la Dar es Salaam, kufanya utafiti wa ufuatiliaji wa uchafuzi wa hewa na kupitia takwimu zilizopo za uchafuzi wa hewa kutoka kwa vihisia (sensor) za ardhini na satelaiti," anasema Dk. Mkiramweni.

Pia anaongeza kwamba mradi ulilenga kupima chembechembe yabisi (microscopic solid) ama matone (liquid droplets) madogo sana, ambayo yanaweza kuvutwa wakati wa kupumua na kusababisha matatizo makubwa ya afya (kwa kitaalamu chembechembe hizi huitwa PM2.5 na PM10).

"Kiwango cha PM kikisoma kuanzia sifuri hadi 50 inakubalika. Ila ikiwa kuanzia 50 na kuendelea hadi 100 kwa wale watu ambao wana shida kiafya inawapa shida. Hutakiwi kukaa eneo hilo zaidi ya saa 24, unatakiwa kuondoka.

"Pugu dampo tulibaini 'sensor' zinasoma 100 na kuendelea maana yake mtu akiishi maeneo hayo kwa muda mrefu inaweza kumletea shida. Daktari anaweza kufafanua, sisi tumechukuwa viwango vya WHO.




Mhadhiri wa DIT, Dk. Mbazingwa Mkiramweni (kulia), akielezea namna vihisia vinavyofanya kazi kwa mmoja wa waliotembelea kwenye Maonyesho ya Sabasaba katika banda la taasisi hiyo. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

> **"Ubora wa hewa katika jiji (mkoa) Dar es Salaam umefuatiliwa kwa kutumia vihisia (sensors) 13 vya gharama nafuu vya PurpleAir PA-II vilivyotumika kuanzia mwezi Mei 2021 mpaka Februari 2022.**

"Kuna maeneo kama Temeke, usiku 'sensor' zinasoma juu pengine ni kutokana na viwanda, labda ni kwa sababu watu wengi wanachoma nyama. 'Sensor' hizi tunazifunga kilomita moja au isipungue mita 500 kutoka eneo unalolenga kulitafiti. Kifaa hiki kinatuma majibu muda wote katika simu na popote."

### HALI ILIVYO

Dk. Mkiramweni anaeleza hali ilivyo katika nchi nyingi za Kiafrika zikirekodi ongezeko la uchafuzi wa hewa, hasa katika miji mikubwa, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo, ukuaji wa viwanda, msongamano wa magari na uchomaji wa taka.

Anasema vihisia vilivyofungwa vilitengenezwa nchini na baadhi kununuliwa kutoka nje na kwamba ilibainika kuwa baadhi ya maeneo, hali ya uchafuzi wa hewa inachangia athari mbaya kwa afya ya binadamu.

"Udhibiti wa uchafuzi wa hewa katika mamlaka ya majiji ni mdogo kutokana mambo tofauti ikiwamo, ukosefu wa data juu ya uchafuzi wa hewa.

"Kukosekana kwa taarifa za maendeleo na utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa ubora wa hewa na sera za udhibiti wa uchafuzi wa hewa. Kwa kiasi kikubwa hii hutokana na uwezo mdogo katika kufanya ufuatiliaji endelevu wa uchafuzi wa mazingira."

Mhadhiri huyo anafafanua kuwa, nchini Tanzania, Dar es Salaam ni moja ya miji inayokua kwa kasi barani Afrika, imepata mafanikio makubwa kwa kuboresha ubora wa hewa.

"Ukuaji wa haraka wa miji na ukuaji wa viwanda umesababisha kuzorota kwa ubora wa hewa katika jiji.

Kupima uchafuzi wa hewa ni hatua muhimu katika kuelewa hatari na kubuni sera madhubuti za kupunguza kiwango cha uchafuzi wa hewa, hivyo kupunguza athari kwa mtu binafsi na jamii, ili kuboresha afya ya umma," anasisitiza.

### DAR YATAMBULIKA

Pia, naeleza athari za uchafuzi wa hewa kwa afya na mazingira jijini Dar es Salaam zimetambuliwa kuwa ni suala muhimu katika ajenda ya mamlaka ya jiji na mipango miji.

"Taratibu za ushirikiano wa kisekta zimekuwa na ufanisi katika kutatua masuala ya kiteknolojia na kiufundi katika nyanja fulani. Kukua kwa kutegemeana kati ya sekta mbalimbali za vyanzo vya uchafuzi wa hewa.

"Katika sekta kama vile viwanda, usafiri, usimamizi wa taka na nyinginezo, kunahitajika mbinu iliyoratibiwa na shirikishi ya kushughulikia suala la uchafuzi wa hewa nchini katika ngazi ya jiji na pia katika ngazi ya kitaifa."

"Ubora wa hewa katika jiji (mkoa) Dar es Salaam umefuatiliwa kwa kutumia vihisia (sensors) 13 vya gharama nafuu vya PurpleAir PA-II vilivyotumika kuanzia mwezi Mei 2021 mpaka Februari 2022.

"Vilipima chembechembe yabisi (microscopic solid) ama matone (liquid droplets) madogo sana ambayo yanaweza kuvutwa wakati wa kupumua na kusababisha matatizo makubwa ya afya (kwa kitaalamu chembechembe hizi huitwa PM2.5 na PM10).

Anasema, mkoani Dar es Salaam, kila siku wastani wa mkusanyiko anauita kitaalamu PM2.5 na PM10 ulirekodiwa katika maeneo yote kwa kutumia vihisia vilivyofungwa wilaya zote tano za mkoa. Hapa mtaalamu huyo anafafanua kuwa:

"Maeneo yaliyofungwa vihisia ni Pugu Dampo, DMDP Magomeni, Madale, Vijibweni Hospitali, Zahanati ya Buza, Makuburi, Ofisi za Manispaa ya Ubungo, Mlimani City, Sinza Hospitali, Ofisi za Manispaa ya Kigamboni, Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam, Shule ya Msingi Vingunguti, na Ofisi za Mazingira Wilaya ya Temeke.

"Viwango vya juu vya PM2.5 na PM10 vilionekana Pugu Dampo (77.26 g/m3 na 90.89 g/m3 g/m3 kwa mfuatano) na DMDP Magomeni (77.25 g/m3 na 94g/m3 kwa mfuatano) ikilinganishwa na vituo vingine.

Wakati Pugu Dampo ni eneo la wazi la kutupa taka la jiji, kituo cha DMDP Magomeni kipo karibu na makutano ya barabarani.

Viwango vya wastani kwa kila siku kwa PM2.5 na PM10 katika vituo vyote kwa kipindi hicho, cha viwango vya juu kwa wastani ilitoka Pugu Dampo (37.94 g/m3) na Shule ya Msingi Vingunguti (47.49 g/m3). Shule ya Msingi Vingunguti, iko eneo la viwanda sehemu ya Wilaya ya Ilala, pia iko karibu na barabara kuu za trafiki na sio mbali na uwanja wa ndege wa kimataifa.

Kwa ujumla, anaeleza kilichobainika ni viwango vingi vilivyorekodiwa kwa wastani wa siku na viwango vya juu vya PM2.5 na PM10 kutoka kwa vituo vya vihisia vilivyopo karibu na barabara zenye magari mengi.

Anataja eneo la kutupa taka za manispaa na katika maeneo ya viwandani huzidi viwango vinavyopendekezwa na WHO ambavyo ni 15 g/m3 kwa PM2.5 na 50 g/m3 kwa saa 24.

### USIKU HEWA CHAFU

Pia data zilizochanganuliwa zinaonyesha uchafuzi hutofautiana katika vituo vya manispaa mchana, ikilinganishwa na usiku viwango huwa juu.

INAENDELEA UK.13

MAZINGIRA

# Migodi midogo inavyoendelea kutikisa maambukizi ya VVU na Ukimwi nchini

INATOKA UK.11

anasimulia Samweli.

Ayub Williamu kutoka mgodi wa Mwabomba Ushetu, anasimulia: "Madada poa wanaofukuzwa mjini, wanakimbilia sehemu zetu za uchimbaji na kwa rangi wanazokuwa nazo, zinawavutia wachimbaji na kuwahonga, kunywa nao vileo na kuingia kwenye ngono zembe bila kutumia kinga... wameambukiziwa VVU na kuwa tegemezi.'

Anatafsiri janga hilo kuwa mwarobani uliokosa tiba, kwa sababu kila mchimbaji anayepata maambukizi hurejea kwenye familia yake, pasipo kueleza kinachomsumbua, hata anaishia kueneza ugonjwa.

### WAMILIKI GESTI BUBU

Sofia Mabula, ni mmiliki wa nyumba za kulala wageni mgodini, akisema anatambua tabia ya wachimbaji wadogo, hata wanawasaidia kwa kuwanunulia kondomu wanazoweka katika vyumba vyao, bado wanakuta hazijatumika.

Anasema, lengo la kuwa na vyumba hivyo sio biashara ya ngono, bali kupumzika wachimbaji watokao shimoni, wakiwalenga wanaotoka mikoa ya mbali, hawana pa kulala, kwa siku wanawatoza Sh.5,000. Chacha Marwa anasema, ilifika hatua akazuia wachimbaji kuingia na wanawake kwenye eneo lake, lakini aliishia kukimbiwa na wateja, sasa amewapa uhuru kufanya wanachohitaji, kwani ni watu wazima.

"Tunanunua kondomu na kuziweka mpokezi na katika vyumba vya kulala lakini hakuna mtu anayetumia na ukikuta imetumika basi huyo atakuwa mchimbaji mpya asiyetumia aina yoyote ya kilevi...Mamlaka zisiwatelekeze wachimbaji ziwafike na kuwaelimisha matumizi ya kinga na kufanya tohara," anasema Marwa.




Kampeni kukabili Ukimwi mkoani Shinyanga. **PICHA: MTANDAO**

### CHAMA WACHIMBAJI

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji wadogo mkoani Shinyanga (SHIREMA), Hamza Tandiko, anasema wamelazimika kuweka mabango katika migodi yote midogo yenye ujumbe wa virusi vya Ukimwi, lengo kuwakumbusha hatari inayowakabili.

Anasema, Ofisi yake inashirikiana na Dawati la Jinsia migodini kuwafikia wachimbaji na kuwaelimisha ngono zembe na maambukizi ya VVU na mimba zisizotarajiwa, akirejea takwimu hadi sasa, hakuna mkasi ulioripotiwa ya mchimbaji kuwapatia mimba wanaojiuza, badala yake ripoti ni za wachimbaji kukimbilia familia zao.

"Mfanyakazi wangu mmoja alitelekeza mke na watoto wawili mapacha baada ya kupata fedha na kujihusisha kwenye ulevi uliokidhiri na ununuzi wa wanawake migodini, suala hili tulilikemea kwa kushirikiana na Dawati la Jinsia, likaisha..." anasimulia Hamza.

Tandiko anasema, kila mwezi migodini, viongozi wao wamekuwa wakitoa elimu ya kujikinga kiafya na wanaokutwa na VVU, kwenda vituoni kuchukua dawa kinga za ARV na huwapatia nauli kurejea kwenye familia zao.

### MRATIBU UKIMWI MKOA

Mratibu wa Ukimwi Mkoa Shinyanga, Dk. Peter Mlacha, anasema mkoa bado umekuwa na ushamiri mkubwa wa maambukizi ya VVU kwa asilimia 5.6, juu ya ushamiri wa Taifa wa asilimia 4.4 na anataja utafiti uliofanywa mwaka 2022/2023 kulinganisha na utafiti wa mwaka 2017/18 ulikuwa asilimia 5.9

Anasema, takwimu nyingi zinaonyesha kushuka kiwango cha maambukizi ya VVU kwa kila kundi la watoto, vijana balehe na watu wazima, huku akitaja maeneo yanoyoongoza kwa maambukizi ni mijini, 'senta' zilizochangamaka kama Kahama, Isaka, Segese, Shinyanga Mjini, Maganzo, vituo vya malori na migodi ya wachimbaji wadogo.

Dk. Mlacha anasema, wanaendelea kuelimisha kinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI, hususani matumizi sahihi ya kondomu, zikihakikishwa zinapatikana maeneo yote ya jamii, wakipitia asasi zisizo za kiserikali, watoa huduma za afya ngazi ya jamii, vituo vya kutoa huduma na vyombo vya habari.

Anasema, huduma za tohara kinga nazo zimeendelea katika maeneo mbalimbali mkoani, hasa halmashauri za Kishapu, Shinyanga Manispaa, Shinyanga Vijijini, Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama, akitaja takwimu mwaka jana 2023, wanaume 8,201 walipata huduma ya tohara kinga, wakiwamo wanaotoka migodni.

Dk. Mlacha anataja kufikia Juni mwaka huu, waliwafikia na kuwahudumia wateja 73,559 kupata dawa za ARV na 1,250 hawakupokea huduma katika kipindi hicho.

Aidha, anataka idadi 11,280 walirejea huduma, huku 40 walihama makazi kimkoa na 30 walitoweka kwa sababu mbalimbali.

# DIT yatafiti uchafuzi hewa Dar, kiwango kinatisha dampo Pugu

INATOKA UK.12

"Tathmini ya Msingi ya Ubora wa Hewa jijini (mkoa) Dar es Salaam, inatoa takwimu muhimu, ili kusaidia uanzishwaji wa malengo ya kupunguza uchafuzi wa hewa, kuandaa mikakati ya kudhibiti uchafuzi wa hewa kutoka sekta muhimu za vyanzo na kuandaa Mpango wa Kudhibiti Ubora wa Hewa katika jiji zima," anasema Dk. Mkiramwemi.

Dk. Mkiramweni anasema Mei mwaka huu, taasisi hiyo ilifanya mazungumzo na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), ili kuja na mradi wa kufunga vihisia hivyo nchi nzima hasa miji mikubwa ili kubaini sehemu yenye tatizo na serikali kuja na mbinu za kukabiliana nayo.

"Utafiti tumeufanya kwanza Dar es Salaam na mashirika yetu yalianza katika majiji kama Nairobi Kenya. Tunawaza kufika Mwanza, Arusha, Mbeya ili kuona kiwango cha uchafu kama kipo maeneo mengine. Taarifa hizi zitasaidia watunga sera, hospitali kujua ugonjwa wa upumuaji kwa nini eneo fulani."

### ATHARI KIAFYA

Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mfumo wa Upumuaji kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Mwanaada Kilima, alipoulizwa na Nipashe, athari za uchafuzi wa hewa kwa binadamu anasema, husababisha kuwapo kwa chembe na kemikali za sumu katika hewa, zikiwamo ukaa, ozoni, daoksaidi ya naitrojeni na salfa.

"Chembe hizi zinapoingia ndani ya mwili wa binadamu, husababisha madhara mbalimbali ya kiafya. Madhara ya muda mrefu na madhara ya muda mfupi," anasema bingwa huyo katika madhara. Anaendelea anasema, yapo ya muda mfupi, kutokana na kuvuta kiwango kikubwa cha hewa chafu ndani ya muda mfupi, hivyo ini pamoja na kikohozi, kifua kubana, kushindwa kuhema vizuri, kizunguzungu, kupoteza fahamu na kifo ndani ya muda mfupi.

Madhara mengine ameyataja ya muda mrefu ni pamoja na magonjwa sugu ya mapafu na mfumo wa upumuaji ikiwamo ugonjwa sugu wa kubana kwa njia za hewa (Chronic Obstructive Pulmonary Dusease).

Pia anataja, shambulio la pumu kila mara hususani kwa watoto. Saratani ya mapafu, kinga dhaifu ya mapafu, inayosababisha maambukizi ya mara kwa mara ya vimelea vya Pneumonia.

"Madhara mengine ni magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, magonjwa ya kisukari na homoni, magonjwa mbalimbali ya ubongo, neva na mfumo wa fahamu, magonjwa ya macho, mimba kuharibika.

Kwa ujumla, uchafuzi wa hewa ni kisababishi kikuu cha pili cha maradhi yasioambukiza duniani na kwa uchafuzi wa hewa ya ndani, makundi yanayoathirika zaidi ni wanawake na watoto, mwanamke anatumia masaa mengi jikoni kila siku na huwa kwenye hatari ya kupumua viwango vikubwa vya hewa chafu itokanayo na nishati tongamotaka.

AFYA

# Mauaji yanapoweka njia panda afya ya akili na mwili wa mtoto

**Na Beatrice Moses**

NCHINI hadi sasa, kuna hofu imetawala kuwapo matukio ya kikatili yakiripotiwa kwenye vyombo rasmi na mazungumzo tofauti, yakihusisha mauaji ya watoto kwenye maeneo tofauti.

Hiyo ni katika kipindi takriban miezi sita, hata kusababisha hofu kwa baadhi ya wazazi na walezi na makundi mengineyo ya malezi ya kijamii. Ushuhuda wake uko pia kwenye mijadala ya mitandao ya kijamii, wazazi na walezi hawana amani.

Ni hali inayojumuisha umma kutawaliwa na hofu inayojengwa na ukweli, familia za watu wa kipato cha kati na chini kumudu ulinzi wa usalama wa watoto saa 24, hasa kwa kuwa ukatili hauna eneo maalum unapotendwa unaweza kuwa shule, njiani au nyumbani.

Miongoni mwa matukio ya kikatili yanatotajwa kutokea ni pamoja na lile linalohusisha dada msaidizi wa kazi za nyumbani, anayedaiwa kumkata shingo mtoto wa mwajiri wake.

Tukio hilo lilitokea Julai 17, 2024, dada huyo kumjeruhi shingoni kwa kitu chenye ncha kali mtoto anayeishi eneo la Goba Kinzudi, Kinondoni kisha mtuhumiwa akadaiwa kukimbia, lakini tayari Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limefanikiwa kumkamata.

Tukio hilo linafuatia mauaji ya mtoto mwenye ualbino, Asimwe, aliyekuwa na umri miaka miwili na nusu yaliyotokea mkoani Kagera. Inadaiwa mtoto huyo alitekwa na watu wasiofahamika Mei 30, 2024 nyumbani kwao kijiji cha Mulamula wilaya ya Muleba mkoani Kagera.

Mwili wa mtoto huyo ulipatikana Juni 17, 2024 ukiwa umenyofolewa baadhi ya viungo. Miongoni mwa watu tisa wanaoshtakiwa kuhusu mauaji ya mtoto huyo, yupo baba mzazi.

Washtakiwa wengine yumo Padre miongoni mwa waliofikishwa mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Bukoba,.

Pia, kuna matukio mengine kadhaa yanayohusisha watoto kutoweka na kukutwa wakiwa wamekufa na kunyofolewa viungo kwenye miili yao.

Ndio katika mazingira kama hayo, hofu inatawala zaidi hasa watu ambao wanatarajiwa kuwa viongozi, wa kuzuia na wakemeaji wa ukatili wanapotajwa kuhusishwa na matukio ya aina hii,

Ni hali inayoibua makundi ya kijamii, bila kujali dini, kabila wala vyama vya siasa, kuunganisha nguvu za pamoja katika kusaka suluhisho la kukomesha vitendo hivyo vya kikatili, vimekuwa vikiibuka zaidi hasa wakati ambapo uchaguzi za viongozi wa kisiasa zinapokaribia.



Watoto katika mijumuiko yao ya asili kufurahi. **PICHA: MTANDAO**

> **Kuna Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi Ya Wanawake na Watoto (Mtakuwa: 2017/18 – 2021/22) ni vyema kuwe na mrejesho mzuri wa utekelezaji wa mpango huu.**

Hilo linajenga mazingira ya viongozi wa kisiasa na serikali za mitaa kujitokeza kuonyesha uwezo wao wa uongozi kwa kuwaunganisha wananchi katika maeneo yao kujadili njia bora ya kuzuia ma kukomesha matukio ya kikatili.

Ni hali watoto wanakosa utulivu na amani kwa habari za matukio hayo, hivyo wanaweza kushindwa kufanya vizuri hata kwenye masomo yao.

Pia kwa baadhi ya wazazi na walezi wa kipato cha kati na cha chini watoto wanakwenda na kurejea kutoka shule wakijitegemea iwe kwa usafiri wa umma au kwa miguu kulingana na umbali wa shule anayosoma mtoto husika nao wanakosa utulivu wa kushiriki vyema kujitafutia kipato.

**SHERIA ZINAKOSIMAMA**

Sheria ya Mtoto Mwaka 2009, ni waraka unaoshughulikia masuala mengi kitaifa yanayohusu haki na ulinzi wa mtoto. Hiyo, pia inachukua mikataba na makubaliano yanayohusu haki za mtoto kwa ujumla.

Inalenga kuimarisha ulinzi, matunzo na haki za watoto nchini hapa, imeainisha haki ya mtoto kulelewa na wazazi, haki ya kupewa jina kuwa na utaifa, haki ya kupata mahitaji ya msingi kama chakula, malazi, mavazi, matibabu, chanjo, elimu, na haki ya kucheza na kuburudika.

Asasi ya World Vision Tanzania, inabainisha kuwa jukumu la ulinzi wa mtoto ulinzi na usalama wa mtoto sio jukumu la maafisa wa ustawi wa jamii peke yao ni jukumu la Taifa kwa ujumla. Hakuna anayeruhusiwa kumdhuru, kumumiza au kumnyonya mtoto.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF), nalo katika katika utafiti uliotolewa Januari 15, 2024 linabainisha kuwa duniani kote mwaka 2024, watoto wanatarajiwa kuona kuongezeka kwa matukio ya ghasia, vita na matatizo ya kiuchumi.

Kila mwanzo wa mwaka, UNICEF huchunguza hatari ambazo watoto wanaweza kukumbana/ kukabiliana nazo, na kupendekeza njia za kupunguza madhara yanayoweza kutokea.

Katika ripoti hiyo inayoitwa Matarajio ya Watoto 2024: Ushirikiano katika Ulimwengu uliogawanyika, pamoja na mambo mengine kadhaa inabainisha katika uchaguzi wa mwaka 2024, na demokrasia ya kimataifa itakabiliwa na hatari ambazo hazijawahi kushuhudiwa, zinazotolewa na taarifa potofu na vurugu za kisiasa, zinazotishia haki na huduma za watoto.

Inaelezwa kuwa watoto na vijana wanaweza kuathiriwa zaidi na unyanyasaji huu, ambao unaweza kusababisha kifo, madhara ya kimwili au ya kihisia, kukatizwa kwa huduma za umma na kufungwa kwa shule, vijana wanaonyesha kutoridhika na demokrasia, lakini wanaelekeza nguvu zao katika hatua za kujenga za kiraia, na uharakati wa mtandaoni.

Pia, kuna athari za ukuaji usiokubalika wa teknolojia ikiwa ni pamoja na zinachochea hofu na wasiwasi kuhusu ustawi wa watoto, sera ya udhibiti unaokuja ikiwa itazingatia mahitaji ya watoto na kubuniwa kwa uwajibikaji, unaweza kutoa fursa na kupunguza athari hasi.

Inaelekeza njia ya kuwalinda watoto, inasema ripoti hiyo, ni mshikamano wa kiuchumi, ushirikiano wa soko, na uwekezaji katika stadi za siku zijazo.

Kuna Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi Ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa: 2017/18 – 2021/22) ni vyema kuwe na mrejesho mzuri wa utekelezaji wa mpango huu.

Imebainishwa kuwa kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2000 Serikali kwa kushirikiana na wadau ilikuwa ikitekeleza mipango nane iliyolenga kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na Watoto, ikiwa ni jitihada za kuleta usawa katika jamii, ambayo pamoja na mafanikio yaliyopatikana kuzuiaa ukatili kwa wanawake na watoto na utoaji huduma kwa waathirika wa vitendo hivyo.

Utekelezaji wa mipango hiyo ulikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upungufu katika uratibu na upatikanaji wa taarifa za uhakika za vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto nchini.

Kwa mujibu wa MTAKUWWA, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiye Mwenyekiti wa Kamati Elekezi ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto Ngazi ya Taifa.

Ni kamati hii inalo jukumu la kutoa miongozo ya kisera na kuratibu utekelezaji wake, pamoja na shughuli za utoaji huduma kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

Katibu wa kamati hioyo ni Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya kusimamia masuala ya Wanawake na Watoto.

Katika hali hiyo, elimu inahitajika, pia na hatua za kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa wazazi wazembe ili watambue wajibu wao wa ulinzi kwa watoto wao, wapo wanaoendekeza anasa na kusababisha watoto kukosa haki ya kulindwa.



## DC Machali aagiza hatua kali wanaowapa mimba wanafunzi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali amewagiza watendaji wa vijiji na kata kuwachukulia hatua za kisheria wazazi watakaobainika kukwamisha kesi za wanafunzi kupewa mimba.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Nkinto ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kata kwa kata kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi, alisema ni lazima watuhumiwa wafikishwe mbele ya vyombo vya sheria.

Alisema tatizo la mimba kwa wanafunzi ni lazima likomeshwe katika Wilaya ya Mkalama na kwamba baadhi ya wazazi wamekuwa kikwazo pale kesi zinapofikishwa mahakamani kwa kukataa kutoa ushirikiano.

"Mzazi yeyote atayebainika kuwa chanzo cha kukwamisha ushahidi mahakamani atachukuliwa hatua za kisheria, mtendaji kuanzia leo ikiwa kuna mzazi anahusika na yeye achukulie hatua za kisheria," alisema Machali.

Aidha, alisema wananchi lazima wawe mstari wa mbele kupinga mimba za utotoni hasa kwa wanafunzi ili kumlinda mtoto wa kike aweze kupata haki ya kusoma.

"Wananchi wenzangu tushirikiane pamoja kupambana dhidi ya tatizo la mimba shuleni, nawaomba sana mtoe ushirikiano pindi kesi za mimba zinapofika mahakamani, wanaume achaneni na wanafunzi," alisema.

Mkuu huyo wa Wilaya akijibu swali lililoulizwa na wananchi kuhusu changamoto ya maji alisema, tayari serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya kuleta maji safi na hata wataalamu kutoka Mamlaka ya Bonde la Maji Mkoa wa Singida wapo Kijiji cha Nkinto kufuatilia vyanzo vya maji.

"Niwahikishishie wananchi wa Kijiji cha Nkinto na vijiji vya jirani kuwa tayari watalaamu wetu wako kazini na nimeambatana nao hapa, kabla ya mwaka huu kuisha mtakuwa mmepata maji," alisema Mahali.

# Benjamin Mkapa yapandikiza uloto kundi tofauti la damu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), imefanikiwa kupandikiza uloto kwa mgonjwa wa sikoseli ambaye mwenye kundi la damu tofauti na mchangiaji.

Mgonjwa huyo ambaye hivi sasa anaendelea vizuri na matibabu hospitalini hapo.

Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Damu BMH, Stella Malangahe, akizungumza jana hospitalini hapo alisema kupitia kitengo chake cha damu salama sasa kina uwezo wa kuchakata uloto uliyotolewa na mchangiaji mwenye kundi tofauti la damu na mpokeaji (mgonjwa), na hivyo kupandikizwa bila kuleta madhara yoyote katika mwili.

Alisema utaalamu huo unaojulikana kama Bone Marrow Manipulation- RBC Depletion ni utaalamu unaofanywa na mashine maalum (apheresis machine) kwa kuchuja na kuchukua uloto uliokusudiwa kisha kumwekea mgonjwa (kumpandikiza) uloto uliobakia.

Alisema wanaishukuru serikali kwa kuwekeza kwenye sekta ya afya jambo linalochangia hospitali kutoa huduma za matibabu ya magonjwa mbalimbali kwa wagonjwa.

"Mgonjwa huyu aliyepandikizwa pamoja na mchangiaji wake wanaendelea vizuri na tayari mgonjwa huyu ameonesha dalili nzuri za kuotesha uloto.

"Mwanzoni tulipoanzisha huduma hii ya upandikizaji uloto hatukuweza kupandikiza uloto kwa mgonjwa mwenye sikoseli anayetofautiana kundi la damu mchangiaji wake, lakini sasa kupitia utaalam huu BMH tunaweza kupandikiza uloto kwa wagonjwa ambao wachangiaji wao wana makundi tofauti ya damu," alisema Dk. Stella.

Alitaja vigezo vingine wanavyozingatia katika upandikizaji uloto mbali na kundi la damu, ambalo sasa limepatiwa ufumbuzi ni pamoja na umri wa mgonjwa (miaka 4 hadi 12), uwepo wa mchangiaji uloto mwenye ufanano wa kinasaba na mgonjwa ( HLA matching) na hali nzuri ya afya ya mgonjwa na mchangiaji uloto.

BMH imekuwa hospitali ya kwanza nchini kutoa huduma hii kwa wagonjwa wa sikoseli na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kutoa huduma hii kwa wagonjwa wa sikoseli.

Huduma ya upandikizaji uloto kwa wagonjwa wa sikoseli ni huduma inayolenga kuondosha kabisa ugonjwa wa sikoseli na kumfanya mgonjwa kupona ugonjwa huu na kurejea katika uimara wa afya kama watu wengine wasio na ugonjwa huo.

Hata hivyo, huduma hii inaendelea kutolewa BMH kwa mafanikio makubwa na hivyo kuendelea kuleta matumaini kwa watanzania wengi, ikizingatiwa kuwa Tanzania ni nchi ya nne duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa sikoseli.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akizungumza na madereva wa bodaboda na bajaji wanaofanya shughuli zao katika stesheni ya treni ya mwendokasi (SGR) ya Mkonze, jijini Dodoma jana, akiwataka kutojiingiza kwenye vitendo viovu, ikiwamo wizi, ulevi na kuwa wasafi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watu 30,000 kushuhudia uzinduzi SGR Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU zaidi ya 30,000 wanatarajiwa kushuhudia tukio la uzinduzi rasmi wa safari za treni ya kisasa ya (SGR) utakaofanywa leo na Rais Samia Suluhu Hassan, katika Stesheni ya mkoa wa Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema maandalizi ya tuikio hilo yamekamilika hivyo wakazi wa mkoa wa Dodoma pamoja na ya jirani wajitokeze kwa wingi kushuhudia tukio la kihistoria.

"Mkoa wa Dodoma umepewa heshima kubwa ya kuandaa tukio hili la kihistoria ambalo kila mmoja wetu anapaswa kushiriki kwani haliwezi jirudia tena,"alisema.

Akizungumzia kuhusu kuanza kwa safari za treni kutoka Dar es Saalam hadi Dodoma, alisema kutasaidia kuufungua mkoa wa Dodoma kiuchumi kwakuwa wafanyabiashara wengi watatumia usafiri huu kupunguza muda wa kufuata bidhaa zao.

"Usafiri huu unakwenda kupunguza muda wa safari ambao watu walikuwa wakitumia hapo awali hivyo mfanyabiashara atakuwa na uwezo wa kwenda Dar es Salaam asubuhi na kurudi jioni akiwa na bidhaa zake tayari,"alisema.

Hata hivyo, aliipongeza serikali kwa kufanikisha kukamilisha ujenzi wa mradi huo mkubwa wa kimkakati ambao utakwenda kuongeza shughuli za kiuchumi na kukuza kipato kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Safari ya kwanza ya treni ya kisasa ya umeme (SGR) kutoka Dar es Saalam kwenda Dodoma ilianza rasmi Julai 25, mwaka huu huku abiria zaidi ya 1,000 wakitumia usafiri huo na wengine kukosa nafasi.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) Masanja Kadogosa, akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuwasili kwa treni hiyo kwa mara ya kwanza alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa maelekezo ya serikali.

"Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo mwaka jana kuwa ifikapo mwezi Julai mwaka huu, lazima usafiri wa treni ya umeme kutoka Dar es Saalam kuja Dodoma uwe umeshaanza rasmi.

"Leo tumetoka Dar es Salaam majira ya 12 asubuhi na kufika Dodoma majira ya saa nne asubuhi na hii ni kutokana na kuwa kuna eneo tulisimama sana kwa ajili ya kupisha na treni iliyotoka huku, lakini kadri siku zinavyokwenda tutaendelea kuboresha changamoto ambazo zimejitokeza leo kama ilivyokuwa wakati tulivyoanza safari za Dar Morogoro,"alisema Kadogosa.

Aidha, alisema katika safari hiyo ya kwanza kuja Dodoma, mwitikio wa abiria kutumia usafiri huo umekuwa mkubwa sana hali ambayo inawapa kazi ya kufanya ili kukidhi mahitaji.

"Leo treni ya asubuhi tayari imejaa na ya jioni na ya kesho pia imejaa hivyo tutaendelea kuangalia mwenendo utakavyokuwa ili kuongeza safari kama ilivyokuwa katika safari za Dar Morogoro,"alisitiza Kadogosa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Spring Oil Limited, S.L.P 2545, Iringa. | Kiwanja Na. 31/3, Kitalu "Industrial Area", Eneo la Kibwabwa, Iringa. | Salim Ahmed Abeid (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 2. | Erasto Yustin Mhongole, S.L.P. 29, Mufindi | Kiwanja Na. 3, Kitalu "C", Eneo la Nyololo, Mufindi, Iringa. | Erasto Yustin Mhongole (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 3. | Obed Jackson Kise T/A Kise Petrol Station, S.L.P 7, Turiani. | Kiwanja Na. 12, Kitalu "B", Eneo la Turiani, Mvomero, Morogoro. | Obed Jackson Kise (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 4. | Furahisha France Msigwa Dodoma, S.L.P 159, Mafinga. | Kiwanja Na. 44, 46, 47 & 48, Kitalu "C", Eneo la Image, Dodoma. | Furahisha France Msigwa (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 5. | Mbuki Eliezer Mbuki, S. L. P 11105, Mwanza. | Kiwanja Na. 322, 323, 324,325 &326, Kitalu "K" Eneo la Malya, Kwimba, Mwanza. | Mbuki Eliezer Mbuki (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 6. | John Chagu Nkono, S. L. P 194, Maswa. | Kijiji cha Mbugamita, Eneo la Senani, Maswa | John Chagu Nkono, (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 7. | Joseph Kando Mkama, S. L. P. 70, Biharamulo, Kagera | Kijiji cha Nyantakara, Biharamulo, Kagera. | Joseph Kando Mkama (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 8. | Johanes Itebuka Tibangabyabo, S. L. P 72, Kyerwa. | Kiwanja Na. 48, Kitalu "F", Eneo la Bugene, Karagwe, Kagera. | Johanes Itebuka Tibangabyabo (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 9. | John Cosmas Jichabu S. L. P 491, Bukoba. | Kijiji cha Migara, Bukoba, Kagera. | John Cosmas Jichabu (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 10. | Petroafrica (T) Limited-Mbulu Two Service Station, S.L.P 4878, Kahama. | Kiwanja Na. 2666, Kitalu "R" Eneo la Mbulu, Kahama, Shinyanga. | Yasin Warsame (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 11. | Tintober Petrol Station, S.L.P 899, Shinyanga. | Kiwanja Na. 34, Kitalu "V" Eneo la Ndembezi, Shinyanga. | Jackton Odera Koyi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 12. | Abel Nestory Sembeka, S.L.P 03, Kakonko. | Eneo la Kikulazo, Rugenge, Kakonko, Kigoma. | Abel Sembeka (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 13. | Nurdin Hassan Babu, S.L.P 5764, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "C", Kilimahewa, Mkuranga, Pwani. | Nurdin Hassan Babu (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 14. | URSA Petrol Station, S.L.P 62453, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 78, Kitalu "F", Eneo la Pangani, Kibaha, Pwani. | Felix Kitua (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 15. | Acer Petroleum (T) Ltd – Mtwara, S.L.P 78845 Dar es salaam | Kiwanja Na. 514, Kitalu "F", Eneo la Msijute, Mtwara. | Atul Mittal (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 16. | Wazo Hill Filling Station, S.L.P 32069, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 297, Kitalu "B", Eneo la Wazo, Kinondoni, Dar es Salaam. | Boniface Nasibu (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 17. | Bagadir Investment Limited, S.L.P. 4646 Dar es Salaam | Kiwanja Na. 1909, Kitalu "BB", Eneo la Chekeni Mwasonga, Kigamboni, Dar es Salaam. | Usamah Mohamed Sheikh (Mtanzania) | Kibali cha ujenzi wa kituo cha mafuta |
| 18. | Seif Ally Rashid, S.L.P 361, Moshi. | Kiwanja Na. 36, Kitalu "A", Eneo la Mabogini, Moshi, Kilimanjaro. | Seif Ally Rashid (Raia wa Tanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 19. | Pilikano Oil Com, S.L.P 89, Mbinga | Kijiji cha Longa, Mbinga, Ruvuma. | Bruno Lambert Kapinga (Mtanznia) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 20. | Washa Luponya Udodi – Washa Investment, S.L.P 2, Namanyere – Nkasi. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Isunta – Namanyere, Nkasi, Rukwa. | Washa Luponya Udodi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 21. | Kawunju BICS Limited, S.L.P 19, Ludewa | Kijiji cha Nsungu, Ludewa, Njombe | Jones Samuel Mapunda (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 22. | Michael Mwaluka Kihaga, S.L.P 1080, Makambako Njombe. | Kiwanja Na. 55, Kitalu "J", Kivavi, Makambako, Njombe. | Michael Mwaluka Kihaga (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 23. | Amos Site Mabena, S.L.P 710, Songea. | Kiwanja Na. 348, Kitalu "N", Majengo, Makambako, Njombe. | Amos Site Mabena (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 24. | Leo Peter Kabarata Mbilinyi T/A Leo Filling Station, S.L.P 166, Morogoro. | Kiwanja Na. 599, Kitalu "L", Barabara ya Msimamo, Eneo la Kihonda,Morogoro. | Leo Peter Kabarata Mbilinyi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Mek One Industries Ltd – Mkamba Filling Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "A", Eneo la Mkamba – Ifakara, Kilombero, Morogoro. | Mohamed Eidha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Oryx Oil Company Ltd – Msamvu, S.L.P. 9540, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 44, Kitalu "E", Eneo la Msamvu, Morogoro. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Acer Petroleum (T) Ltd – Morogoro, S.L.P 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "D", Eneo la Kingolwira, Morogoro. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Lake Oil Ltd-Dodoma Kisasa Service Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "E", Eneo la Kisasa, Dodoma. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Oilcom Soya Petrol Station, S.L.P 80, Kiteto | Kijiji cha Soya, Chemba, Dodoma. | Amin Habib Punja (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | Mrijo Petrol Station, S.L.P 80, Kiteto. | Kijiji cha Mrijo Chemba, Dodoma. | Amin Habib Punja (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 31. | Jafari Rajabu Guka T/A Soya Filling Station, S.L.P 174, Kondoa. | Kijiji cha Soya, Chemba, Dodoma. | Jafari Rajabu Guka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | Valentino Edwardi Nywage Pandambili, S.L.P 57, Kongwa. | Eneo la Pandambili, Kongwa,Dodoma. | Valentino Edwardi Nywage (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "AB", Eneo la Medeli Dodoma. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | Lake Oil (T) Ltd – Nala Dodoma Service Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 119, Kitalu "A", Eneo la Nala, Dodoma. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "P", Mafinga, Mufindi, Iringa. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Falcon Trans and Oil Company Limited, S.L.P 839, Iringa. | Kiwanja Na. 21, Kitalu "Zone II", Eneo la Gangilonga, | Saleh Mansoor Huwel (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | Mohamed Jama Saad, S.L.P 198, Meatu – Simiyu | Kijiji cha Ibaga, Mkalama, Singida. | Mohamed Jama Saad (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Mkumbo Daniel Ramadhani T/A MDR Oil, S.L.P 88, Hungumalwa. | Kiwanja Na. 171, Kitalu "A", Eneo la Hungumalwa, Kwimba, Mwanza. | Mkumbo Daniel Ramadhani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 39. | GBP Tanzania Limited, S.L.P 6185, Mwanza. | Kiwanja Na.442, Kitalu "A", Eneo la Nyamhongolo, Mwanza. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 40. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.15, Kitalu "C", Eneo la Mabatini, Mwanza. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41. | Sereniva Company Limited, S.L.P 872, Musoma. | Eneo la Igombe, Ilemela, Mwanza. | Christopher Stephen Matthew (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

# TANGAZO

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 21. | Kawunju BICS Limited, S.L.P 19, Ludewa | Kijiji cha Nsungu, Ludewa, Njombe | Jones Samuel Mapunda (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 22. | Michael Mwaluka Kihaga, S.L.P 1080, Makambako Njombe. | Kiwanja Na. 55, Kitalu "J", Kivavi, Makambako, Njombe. | Michael Mwaluka Kihaga (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 23. | Amos Site Mabena, S.L.P 710, Songea. | Kiwanja Na. 348, Kitalu "N", Majengo, Makambako, Njombe. | Amos Site Mabena (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 24. | Leo Peter Kabarata Mbilinyi T/A Leo Filling Station, S.L.P 166, Morogoro. | Kiwanja Na. 599, Kitalu "L", Barabara ya Msimamo, Eneo la Kihonda, Morogoro. | Leo Peter Kabarata Mbilinyi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Mek One Industries Ltd – Mkamba Filling Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "A", Eneo la Mkamba – Ifakara, Kilombero, Morogoro. | Mohamed Eidha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Oryx Oil Company Ltd – Msamvu, S.L.P. 9540, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 44, Kitalu "E", Eneo la Msamvu, Morogoro. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Acer Petroleum (T) Ltd – Morogoro, S.L.P 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "D", Eneo la Kingolwira, Morogoro. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Lake Oil Ltd-Dodoma Kisasa Service Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "E", Eneo la Kisasa, Dodoma. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Oilcom Soya Petrol Station, S.L.P 80, Kiteto | Kijiji cha Soya, Chemba, Dodoma. | Amin Habib Punja (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | Mrijo Petrol Station, S.L.P 80, Kiteto. | Kijiji cha Mrijo Chemba, Dodoma. | Amin Habib Punja (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 31. | Jafari Rajabu Guka T/A Soya Filling Station, S.L.P 174, Kondoa. | Kijiji cha Soya, Chemba, Dodoma. | Jafari Rajabu Guka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | Valentino Edwardi Nywage Pandambili, S.L.P 57, Kongwa. | Eneo la Pandambili, Kongwa, Dodoma. | Valentino Edwardi Nywage (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "AB", Eneo la Medeli Dodoma. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | Lake Oil (T) Ltd – Nala Dodoma Service Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 119, Kitalu "A", Eneo la Nala, Dodoma. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "P", Mafinga, Mufindi, Iringa. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Falcon Trans and Oil Company Limited, S.L.P 839, Iringa. | Kiwanja Na. 21, Kitalu "Zone II", Eneo la Gangilonga. | Saleh Mansoor Huwel (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | Mohamed Jama Saad, S.L.P 198, Meatu – Simiyu | Kijiji cha Ibaga, Mkalama, Singida. | Mohamed Jama Saad (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Mkumbo Daniel Ramadhani T/A MDR Oil, S.L.P 88, Hungumalwa. | Kiwanja Na. 171, Kitalu "A", Eneo la Hungumalwa, Kwimba, Mwanza. | Mkumbo Daniel Ramadhani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 39. | GBP Tanzania Limited, S.L.P 6185, Mwanza. | Kiwanja Na.442, Kitalu "A", Eneo la Nyamhongolo, Mwanza. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 40. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.15, Kitalu "C", Eneo la Mabatini, Mwanza. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41. | Sereniva Company Limited, S.L.P 872, Musoma. | Eneo la Igombe, Ilemela, Mwanza. | Christopher Stephen Matthew (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 60. | Mount Meru Petroleum Ltd – Mbezi Luis, S.L.P 7094, Arusha. | Kiwanja Na. 1709, Kitalu "A", Eneo la Mbezi Luis, Ubungo, Dar es Salaam. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 61. | August Alphonce Ngowi T/A Esther Filling Station, S.L.P 67315, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P21040, Mbezi Msumi, Ubungo, Dar es Salaam. | August Alphonce Ngowi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 62. | Lake Oil Ltd – Pugu Mwakanga Petrol Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2229, Kitalu "A", Eneo la Pugu Mwakanga, Ilala, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 63. | Lake Oil Mwananyamala Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P23732, Eneo la Mwananyamala Mwakanga, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 64. | Thunderbolt Group Limited, S.L.P 13745, Arusha. | Kiwanja Na. 421, Kitalu 3, Eneo la Eneo la Makongo Juu, Kinondoni. Dar es Salaam. | Abel Japhet Lema (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 65. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2083, Kitalu "D", Eneo la Chamanzi, Temeke, Dar es Salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 66. | Big Bon Shopping Centre Sinza, S.L.P 21531, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 27, Eneo la Mbagala, Temeke, Dar es Salaam. | Mohamed Salim Bahashwan (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 67. | Olympic Petroleum (T) Ltd -Toangoma Service Station, S.L.P.16484, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1002, Eneo la Toangoma, Temeke, Dar es Salaam. | Ally Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 68. | Esther Filling Station, S.L.P 67315, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1199, Kitalu "K", Ubungo, Dar es Salaam. | Augustino Alphonce Ngowi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 69. | Top Oil Petroleum Limited, S.L.P 42445, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2193, Kitalu "E", Gongo la Mboto, Ilala, Dar es Salaam. | Mbarak Salim Bawazir (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 70. | Pyramid Oil Company Limited – Chanika, S.L.P 2473, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P35108, Eneo la Buyuni, Ilala, Dar es Salaam. | Sebastian John Luena (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 71. | Nyakyame Co. Limited – Kimanzichana, S.L.P 8326, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 27, Kitalu "B", Eneo la Kimanzichana, Mkuranga, Pwani. | Joseph Kyalo Mwita (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 72. | FSS Fuel Service Station, S.L.P 42202, Dar es Salaam. | Eneo la Mdaula, Chalinze, Pwani. | Saad Fuad Saad (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 73. | Mtwara Bulk Storage Terminal Ltd, S.L.P 1419, Mtwara. | Kiwanja Na. 1, Eneo la Bandari Road, Mtwara. | Leon William Mazigo (Mtanzania) | Leseni ya *Condensate Dealership* |
| 74. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 28, Kitalu "A", Malopokelo, Tandahimba, Mtwara. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 75. | Imani Abeid Haule, S.L.P 55011, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 468, Kitalu "E", Ludewa, Njombe. | Imani Abeid Haule (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 76. | Acer Petroleum (T) Ltd- Makambako, S.L.P 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 148, Kitalu "H", Eneo la Makambako, Njombe. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 77. | Saatatu Investment Limited, S.L.P 14, Mbozi. | Viwanja Na. 70 & 71, Kitalu "B", Lubele-Ibanda, Kyela, Mbeya. | Yona Saatatu Chaula (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 78. | Njombe Filling Station Company Limited – Isanga, S.L.P 411, Njombe. | Kiwanja Na. 11, Kitalu "J", Isanga, Mbeya. | James Malika Mwinuka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 79. | Summer Estate Limited, S.L.P 702, Mbeya. | Kiwanja Na. 1454, Eneo la Ushirika, Rungwe, Mbeya. | John Johnson Summer (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 80. | Nyasa Fuels Limited, S.L.P 147, Songea. | Kiwanja Na. 59, Eneo la Viwandani, Songea, Ruvuma. | Andrew Mpembo Nyirenda (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 81. | Abed Justin Chikila – Chikila Investments, S. L. P 114, Songea. | Kijiji cha Mkeke, Mbinga, Ruvuma. | Abed Justin Chikila (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 82. | Gapco Tanzania Limited, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 191, Kitalu "L", Eneo la Mwaka – Tunduma, Momba, Songwe. | Mamadou Ngom (Senegal) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 83. | Manyanya Oil Limited – Mlowo, S.L.P 132, Tunduma. | Kiwanja Na. 12, Kitalu "C", Mlowo, Mbozi, Songwe. | Bahati Msajie Mnozya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Jengo la EWURA, 3 MTAA WA EWURA., 41104 Tambukareli**
**P.O Box 2857, Dodoma**
**Tel: +255-26 2329003-3; Fax: +255-26 2329005;**

**Toll-Free 0800110030**
**Email: info@ewura.go.tz Website: www.ewura.go.tz**

Imetolewa na:

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 18017 OF 2024
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE
GABRIEL JACOB MUYA
AND IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION

BY JACOB GABRIEL MUYA

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23RD day of August .2024
Dated at KOROGWE this 30TH day of July.2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 17779 OF 2024
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FRANCIS JOHN ALPHONCE
AND IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION
BY SERAPIA ALPHONCE MACHA

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23RD day of August .2024
Dated at KOROGWE this 30TH day of July.2024

RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE DISTRICT

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
INAYOKETI MWANZA
SHAURI LA RUFAA YA MADAI NAMBA 334 LA MWAKA 2021
NYANZA ROAD WORKS LIMITED....MRUFANI
DHIDI YA
HARMONY CREATE GROUP COMPANY LIMITED...MJIBU RUFAA WA KWANZA
NGUBO MUNGIA DIWANI...MJIBU RUFAA WA PILI

**KWA: NGUBO MUNGIA DIWANI**
**KUITWA SHAURINI**
UNAJULISHWA KWAMBA SHAURI LA RUFAA YA MADAI TAJWA HAPO JUU LIMEPANGWA KUSIKILIZWA NA MAHAKAMA HII HAPA MWANZA TAREHE 14/08/2024 SAA TATU KAMILI ASUBUHI (3:00). UNATAKIWA KUHUDHURIA WEWE BINAFSI AU WAKILI WAKO KISHERIA.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO KWA TAREHE TAJWA, KESI HII ITAENDELEA KUSIKILIZWA BILA WEWE KUWEPO MAHAKAMANI NA KUTOLEWA MAAMUZI.
HATI HII IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 22/07/2024

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATRICE HENRY NHOGUTI**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T852DUN aina ya TOYOTA TOWNACE, Chassis No. KM851000608, Engine No. 7K0765007 Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/DOD/32200/2024**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI
Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA
Shauri la Madai Na. 274/2024
JINA LA MDAI ........... JOHNSON RWEGASILA MUTABUZI
JINA LA MDAIWA ................... LUHAGA MPINA

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**KWA**
**LUHAGA MPINA**
**DODOMA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TSH. 3,996,300/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 01 mwezi 08 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku yaM kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 23 Mwezi 07 Mwaka 2024.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIUS DANIELY LYIMO**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari Suzuki Escudo yenye namba za usajili T 665 ABT.
CHASSIS NO TA01W802920 NA ENGINE NO G16A110254
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi .
**TAARIFA YA POLISI:**
**PHQ/KIL/MOS/ 15282/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEX BARAKA KENGA**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina la umiliki wa **MAMA SAVANA SAFARI'S COMPANY LIMITED** yenye namba za usajili **T 691 BYV** aina ya **TOYOTA LANDCRUISER**. Chassis namba **JTELB71J607095125.** Engine namba **1HZ0682654.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/ARU/ARU/26657/2024.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOSES SAMWEL KALINGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye index namba 1941513 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupita **SHULE YA MSINGI KILIMAHEWA** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/RUK/SUM/1521/2024**

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Rais Ruto apokea ripoti mauaji ya Shakahola

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, amepokea ripoti kutoka kikosi kazi kilichoundwa kufuatia mauaji ya Shakahola, ikipendekeza kuanzishwa kwa ofisi ya Msajili wa Mashirika ya Kidini ili kuboresha mifumo ya utoaji taarifa na utekelezaji.

Akiwasilisha ripoti hiyo jana, kiongozi wa timu hiyo, Mutava Musymi, alisema mapendekezo hayo yanatokana na maoni ya Wakenya na wadau mbalimbali waliohojiwa nchini kote.

Katika mapendekezo hayo, ilitaka chombo hicho kiwe na kazi ya kuhakiki utoaji wa taarifa wenye ufanisi, kurahisisha uingiliaji kati kwa wakati ili kusaidia kuzuia madhara yanayoweza kutokea na kutetea ustawi wa jamii.

Alisema ripoti hiyo inapendekeza ofisi hiyo itachukua jukumu muhimu katika kupunguza misimamo mikali ya kidini, imani na mila za uchawi nchini humo.

Kikosi kazi hicho kilianzishwa ili kubaini changamoto za kisheria, kitaasisi na kiutawala zinazoweza kusababisha ukuaji wa mashirika, madhehebu na madhehebu yenye misimamo mikali ya kidini, na kutoa mapendekezo ya kuzuia vitendo vinavyoharibu afya ya umma, usalama na maadili ya taifa.

"Ofisi inayopendekezwa itaunda na kutekeleza njia iliyojumuishwa na iliyowezeshwa kiteknolojia ya kuripoti. Hii itajumuisha nambari za simu za dharura bila malipo, majukwaa ya mitandao ya kijamii, majukwaa ya mtandaoni, programu za wavuti na imu," ilipendekeza rpoti hiyo.

Timu hiyo pia ilisisitiza kuundwa kwa Tume ya Masuala ya Kidini ili kudhibiti maudhui ya kidini kwenye vyombo vya habari kwa kushauriana na Mamlaka ya Mawasiliano, vyombo vya usalama na taasisi za kidini.

Aidha, alisema wameandaa Rasimu ya Mswada wa Mashirika ya Kidini wa 2024 na Rasimu ya Sera ya Mashirika ya Kidini ambayo itasaidia kusisitiza na kuweka mapendekezo ya ripoti hiyo kuwa ya kitaasisi.

Musyme alisema, mapendekezo hayo yanalenga kulinda na kulinda uhuru wa dini na kupunguza matumizi mabaya yanayoweza kuwadhuru Wakenya.

Mapendekezo mengine ni pamoja na haja ya kurekebisha mitaala ya elimu ya msingi ili kuimarisha uvumilivu wa kidini, kutahadharisha umma dhidi ya misimamo mikali ya kidini na kuangalia nyenzo za elimu ya uraia kuhusu haki na wajibu wa mashirika ya kidini na wananchi.

**Radio Jambo**

MAUAJI YA ISMAIL HANIYEH

# Hamas, Iran waapa kulipa kisasi, hofu yazidi Mashariki ya Kati

**TEHRAN,** Iran

HALI ya wasiwasi imetanda eneo la Mashariki ya Kati, kufuatia mauaji ya kiongozi mkuu wa kundi la Hamas, Ismail Haniyeh, yaliyotokea nchini Iran.

Taarifa iliyotolewa na kundi hilo ilisema Haniyeh aliuawa jana katika shambulizi la anga linalodaiwa kufanywa na Israel kwenye makazi yake katika jiji la Tehran.

Kulingana na kundi hilo, Haniyeh alifariki baada ya kushiriki sherehe za kuapishwa kwa Rais mpya wa Iran, Masoud Pezeshkian, iliyofanyika Jumanne.

Hata hivyo, hadi sasa hakuna aliyekiri kuhusika na mauaji hayo.

Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Iran, lilisema chanzo cha shambulizi hilo hakijafahamika na wanaendelea kufanya uchunguzi.

Kundi hilo la Hamas linalodhibiti Ukanda wa Gaza lilisema mauaji ya Haniyeh ni sawa na uhaini.

Mauaji ya kiongozi huyo mkuu wa Hamas, yameleta wasiwasi baada ya kuibuka vita vya pande zote katika Mashariki ya Kati kuliko wakati mwingine wowote.

Nader Hashemi, ambaye ni profesa wa Masomo ya Mashariki ya Kati katika Chuo Kikuu cha Georgetown, aliiambia BBC, kuwa hilo ni tukio kubwa na linaathiri pia matukio ya mvutano uliokuwapo Lebanon, kutokana na saa chache baada ya tukio hilo Israel ilijaribu kumuua kiongozi mkuu wa Hezbollah Fuad Shukr, kusini mwa mji wa Beirut.

Alisema mauaji ya Haniyeh yamebadilisha mtazamo huo, kwani Iran sasa imepata sababu ya kupanua mzozo huo.

Rais wa Mamlaka ya Palestina, Mahmoud Abbas, amelaani mauaji ya Haniyeh akiita kama kitendo cha woga na tukio hatari.

Katika taarifa yake iliyotolewa na Shirika la Habari la Palestina (Wafa), alitoa wito kwa Wapalestina kuungana na kuwa na subira na imara wakati wa uvamizi kutoka kwa Israel.

Jeshi la Ulinzi la Mapinduzi ya Kiislamu ya Iran (IRGC) lilitoa salamu za rambirambi, kufuatia kifo cha Ismail Haniyeh.

Taarifa iliyotolewa na chombo chake cha habari cha Sepah news, ilisema bado inachunguza sababu na ukubwa wa tukio na itatangaza kile ilichobaini baadaye.

Iliongeza kuwa kiongozi huyo aliuawa na walinzi wake.

IRGC ni kikosi kikubwa cha kijeshi kinachoambatana na siasa na uchumi nchini Iran, na kina uhusiano wa karibu na kiongozi mkuu, Ayatollah Ali Khamenei.

Israel iliapa kumuua Haniyeh na viongozi wengine wa Hamas kutokana na kuhusika na shambulio la Oktoba 7, mwaka jana ndani ya nchi hiyo na kuua watu 1,200 na wengine 250 kuchukuliwa mateka.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) liliviambia vyombo vya habari ikiwamo CNN na shirika la habari la Agence France, kwamba halitajibu ripoti zinazotolewa na vyombo hivyo kuhusu kifo cha Haniyeh.

Israel mara nyingi haifanyi hivyo linapokuja suala la mauaji yanayotekelezwa na shirika lao la kijasusi la Mossad.

Kabla ya kifo chake, kiongozi huyo aliwaambia baadhi ya viongozi wa Iran, kuwa kadhia ya Palestina ina gharama na wako tayari kwa gharama hizo kuuawa kama shahidi kwa ajili ya Palestina, Mwenyezi Mungu, na kwa utukufu wa taifa lao.

Israel haijatoa tamko rasmi kuhusu kifo cha Haniyeh lakini kumekuwa na hisia kutoka kwa baadhi ya wanasiasa kama Waziri wa Turathi Amichay Eliyahu, ambaye ameonekana kufurahia.

Kupitia mtandao wa X, aliandika kwamba kifo cha Haniyeh kinaifanya dunia kuwa mahali salama.

"Hii ndiyo njia sahihi ya kusafisha dunia kutokana na uchafu huu. Hakuna tena maafikiano ya amani ya kufikirika au makubaliano ya muda, hakuna tena huruma kwa wanadamu hawa". Aliandika Eliyahu.

Pia alisema kile watakachopitia kitaimarisha uwezo wa kuishi kwa amani na wale wanaotaka amani.

**Wakati huo huo, Jeshi la Ulinzi la Israel**

Ofisa Mkuu wa Hamas ameapa kwamba kundi hilo litajibu mapigo kwa mauaji ya kiongozi wao.

Moussa Abu Marzouk ametaja shambulizi hilo kuwa ni kitendo cha woga ambacho hakitapita bila kulipizwa kisasi.

Kulingana na televisheni ya Al-Aqsa inayoendeshwa na Hamas, Marzouk, alisema wapo tayari kulipiza kisasi.



**Iran yakasirishwa**

Israel na Iran zimekuwa katika vita nyuma ya pazia kwa muda mrefu na mara nyingi zikishambuliana bila kukiri nani kuhusika.

Hata hivyo, Iran inaamini kuwa Israel kwa mara kadhaa imefanya mauaji kadhaa yaliyolengwa katika ardhi yake.

Baadhi ya kesi zinazojulikana zaidi ni pamoja na kuuawa kwa mwanasayansi mkuu wa nyuklia wa Iran, Mohsen Fakhrizadeh, ambaye alipigwa risasi kwa kutumia silaha za kuongozwa na vifaa maalumu mnamo 2021, na kupigwa risasi kwa Kamanda wa Kikosi cha Ulinzi wa Mapinduzi ya Iran, Kanali Sayad Khodai, jijini Tehran mnamo Mei, 2022.

**Viongozi waliouawa**

VIONGOZI kadhaa wa Hamas wanaaminika kuuawa na Israel tangu wakati huo, akiwamo kiongozi wa kisiasa Saleh al-Arouri na Marwan Issa, ambaye ni Naibu Kamanda wa Tawi la Kijeshi la Hamas.

Watoto watatu wa Ismail Haniyeh na wajukuu zake wanne pia waliuawa katika shambulizi la anga lililofanywa na Israel Ukanda wa Gaza mnamo Aprili, mwaka huu.

Hata hivyo, Msemaji wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari, alisema kwamba hakuna mabadiliko katika sera ya ulinzi wa kuilinda nchi hiyo.

Katika chapisho lake kwenye mtando wa X, aliandika kwamba IDF inafanya tathmini ya hali ilivyo. Ikiwa mabadiliko yoyote yataamuliwa, itatoa taarifa kwa umma mara moja.

**Russia, Uturuki zalaani**

Russia na Uturuki yamekuwa mataifa ya kwanza kulaani mauaji ya kiongozi wa Hamas.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia, ilielezea mauaji ya Haniyeh kama mauaji yasiyokubalika kisiasa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mikhail Bogdanov, alisema kifo cha kiongozi wa Hamas kitasababisha kuongezeka kwa mvutano.

Wakati huo huo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uturuki, pia ilisema mauaji hayo ni aibu.

Taarifa iliyonukuliwa na Reuters, ilisema kwamba shambulio hilo pia linalenga kueneza vita vya Gaza katika mwelekeo wa kikanda.

**Ismail Haniyeh ni nani?**

Ismail Haniyeh, alizaliwa katika kambi za wakimbizi zilizoko Ukanda wa Gaza mwaka 1963, alikuwa mwanachama muhimu wa Hamas tangu kuanzishwa kwa kundi hilo.

Haniyeh alifungwa na Israel mara kadhaa na wakati fulani alifukuzwa kwenda kuishi ukimbizini Lebanon kusini kwa miezi sita.

Mnamo 2003, alinusurika jaribio la kuuawa na Israel, akiwa pamoja na mwanzilishi wa Hamas.

Miaka mitatu baadaye, alikuwa Waziri Mkuu wa Palestina kwa muda mfupi baada ya Hamas kushinda uchaguzi, lakini mpasuko kati ya Hamas na Fatah, ulifuata nafasi hiyo mwaka mmoja uliofuata.

Hata hivyo, kutokana na uelewa wake wa uhalisia wa mambo, Haniyeh alidumisha uhusiano mzuri na vikundi vingine hasimu vya Palestina.

Alichaguliwa kuwa mkuu wa ofisi ya kisiasa ya Hamas mwaka 2017.

Katika miaka ya hivi karibuni, aliishi uhamishoni katika nchi za Uturuki na Qatar.

Kiongozi huyo alikuwa nguzo muhimu katika mazungumzo juu ya mpango wa kusitisha mapigano katika Ukanda wa Gaza.

**BBC**

# MASHUJAA YATAJA SABABU YA KUPIGA KAMBI YAKE DAR

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mashujaa imesema viwanja vingi vya mazoezi, maeneo ya mazoezi ya 'gym' za kisasa na kuwepo kwa timu nyingi kubwa ndiyo sababu iliyowafanya waweke kambi yao ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Meja Abdul Mbaraka, amesema watarejea kwao Kigoma mara baada ya kumalizika kwa 'pre season', lakini kwa sasa wataendelea kuwa Dar kwa sababu kuna mahitaji mengi ambayo yanakidhi kwa kambi kuliko wangebaki Kigoma.

"Tuko Dar es Salaam kwa sababu huku kuna vitu vingi sana, viwanja vingi vya mazoezi, kumbi nyingi za kisasa za 'gym', pia kuna timu nyingi hivyo tunaweza kupata mechi nyingi za kujipima nguvu kirahisi na zilizo kwenye levo yetu, tumekuja hapa na kuzikuta timu nyingi hata za Ligi Kuu ambazo zipo 'pre season'," alisema mwenyekiti huyo.

Alitolea mfano kuwa wiki iliyopita walicheza dhidi ya Prisons ambayo nayo iko jijini Dar es Salaam kwa maandalizi ya msimu, ingawa walifungwa bao 1-0, lakini walipata mechi nzuri ya kujua makosa ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi haraka.

"Tuliikuta Prions hapa tukacheza nao mechi ya kirafiki, tulifungwa bao 1-0 na siyo hiyo tu, kuna timu nyingi sana za Ligi Kuu zipo hapa Dar es Salaam ambazo zimepiga kambi, na kwa taarifa tu mechi ya pili tutacheza dhidi ya KMC, faida zote hizi tumezipata kwa sababu ya kuwa Dar," alisema Meja Abdul.

Timu hiyo inayonolewa na kocha Mohamed Abdallah 'Bares' iliyomaliza nafasi ya nane msimu uliopita ikivuna pointi 35, imefanya usajili mkubwa kueleka msimu ujao, ikiwanasa Seif Karihe kutoka Mtibwa Sugar, Chrispin Ngushi wa Yanga, Abdulmalik Zacharia akitokea Namungo,nyota wa zamani wa Simba, Mohamed Mussa, Carlos Protus, Mathew Michael, Ismail Mgunda, Robert Mathias na Ally Nassor 'Ufudu'.

## *Simba Queens yasomba wachezaji Yanga Princess*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya tetesi za muda mrefu, klabu ya Simba imetangaza rasmi kuwasajili wachezaji wapya watatu kutoka timu ya soka ya wanawake ya Yanga Princess ambao wamemaliza mikataba yao na klabu hiyo.

Wachezaji wao ni raia wawili wa Nigeria, kiungo mshambuliaji, Precious Christopher, kiungo mkabaji Saiki Atinuke na beki wa kushoto rai wa Kenya, Wincate Kaari. Wachezaji hao wametambulishwa siku moja tu baada ya kumsajili mchezaji Amina Bilal kutoka JKT Queens na timu ya taifa ya Tanzania, Twiga Stars.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo inasema usajili huo unafanywa kwa lengo wa kukiimarisha kikosi hicho kitakwenda Ethiopia mwezi ujao kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika kanda ya Afrika Mashariki na Kati, CECAFA, inayotarajiwa kuanza Agosti 17, huku ikitarajiwa kuanza kampeni yake hiyo, Agosti 18 itakapocheza dhidi ya FAD ya Djibouti.

Precious, Saiki na Wincate, walikuwa moja ya wachezaji walioibeba sana Yanga Princess Ligi Kuu msimu uliopita kutokana na uwezo mkubwa waliouonyesha licha ya kwamba haikuweza kutwaa ubingwa.

Mbali na wachezaji hao, Simba Queens imetangaza pia kuwasajili wachezaji wengine wapya ambao ni Emiliana Isaya kutoka Ceasia Queens na Josephine Julias kutoka Baobab Queens. Wachezaji hao wote wanasajili ili kuziba nafasi za wachezaji 10 ambao wamechwa kuelekea msimu ujao.

Wachezaji waliopewa mkono wa kwaheri kwenye kikosi hicho sita wa Kitanzania na wanne wa kigeni ni, golikipa Zubeda Mgunda, Zainamu Mohamed, Koku Kipanga, Wema Richard, Silvia Thomas, na Diana Mnally ambaye aliwahi kukichezea kikosi cha timu ya taifa ya Tanzania, Twiga Stars.



Wachezaji wa Timu ya Kiwalani FC, Shaban Abdull (mbele), akimtoka mchezaji mwenzake, Michael Peter, wakati wa mazoezi ya timu hiyo jana kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Kiwalani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## KVZ yapania ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa klabu ya KVZ FC umesema unajipanga msimu ujao waweze kutwaa ubingwa wa Ligi kuu ya Zanzibar baada ya kuukosa kwa misimu miwili mfululizo.

KVZ FC katika msimu wa 2022-2023 ilimaliza nafasi ya pili wakati msimu wa 2023-2024 ilimaliza nafasi ya nne.

Akizungumza na gazeti hili juu ya mipango ya timu hiyo kuelekea msimu mpya, Meneja wa timu hiyo, Abdi Kombo, alisema wangependa kuwa na msimu wenye mafanikio na kutimiza lengo lao la kutwaa ubingwa

Alisema katika kuhakikisha wanafikia malengo yao msimu huu, timu hiyo itakuwa na jumla ya wachezaji 28 ambao wanamatumaini makubwa ya kufanya vizuri.

Alisema kati ya wachezaji hao 28, mpaka sasa jumla ya wachezaji 21 tayari wameshaanza mazoezi ya kujiandaa na msimu wa Ligi Kuu huku wengine saba wakitarajiwa kujiunga na timu hiyo wakati wowote kuanzia sasa.

Alisema kati ya wachezaji hao wachezaji nane ni ingizo jipya ambao wamewasajili msimu huu huku wachezaji watano wakitoka nje ya Tanzania Bara na wachezaji watatu kutoka katika Klabu za Zanzibar.

"Tumefanya usajili kwa mujibu wa matakwa ya mwalimu wetu kulingana na kikosi chetu kwa msimu uliopita lakini pia safari yetu kuelekea msimu ujao, lengo ni kuona tunakuwa na msimu wenye mafanikio zaidi" alisema.

Aidha alisema kuwa timu hiyo inatarajia kucheza mchezo wake wa kwanza wa kirafiki dhidi ya timu ya Polisi inayoshiriki ligi daraja la kwanza.

Alisema katika mchezo huo ndio utampa mwanga na taswira kocha mkuu wa timu hiyo kuangalia kikosi chake hasa kwa wachezaji wapya waliowasajili.

Hata hivyo Meneja huyo amewataka mashabiki wa timu hiyo kuamka kihamasa kama ikivyokuwa msimu uliopita ili wachezaji waweze kufanya vizuri.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA NA LUKAKU

CHELSEA inajadili mpango wa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, kujiunga na Napoli, huku mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, akitarajiwa kuhamia klabu hiyo kwa mkopo. ***(Athletic)***

### GROSS HUYOOO DORTMUND

KLABU ya Brighton imekubali mkataba wa pauni milioni 5.9 kumruhusu kiungo wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross mwenye umri wa miaka 33, kujiunga na Borussia Dortmund. (***Guardian)***

### RABIOT KUTUA UNITED

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, anakaribia kusaini Manchester United baada ya kuondoka Juventus mwishoni mwa mkataba wake. ***(Mail)***

### SETFORD ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kumsajili mlinda mlango wa Uingereza, Tommy Setford mwenye umri wa miaka 18, kutoka Ajax kabla ya ziara yao ya kwenda Marekani. ***(Evening Standard)***

### LINDSTROM MKOPO EVERTON

KIUNGO wa kati wa Denmark, Jesper Lindstrom, mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kucheza kwa mkopo wa msimu mzima pale Everton kutoka Napoli. ***(CalcioMercato)***

### GOMEZ AWINDWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imefanya mazungumzo na Inter Miami kuhusu mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Paraguay, Diego Gomez, 21. ***(Sky Sports)***

### HARRIS ATAJWA BIRMINGHAM

KLABU ya Birmingham City imeelekeza macho yao kwa kiungo wa Fulham na Wales, Luke Harris, 19. ***(Football Insider)***

### KANTE KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mdomo ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante, 33, kutoka Al Ittihad. ***(The Athletic)***

### DIGNE KUUZWA VILLA

ASTON Villa inajiandaa kumuuza mlinzi wa Ufaransa, Lucas Digne, 31. ***(Football Insider)***

### UGARTE SAFI NA UNITED

KIUNGO wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte, 23, amekubaliana maslahi binafsi na Manchester United, ambao wanaendelea kufanya mazungumzo na Paris St-Germain. (***Fabrizio Romano)***

### MCTOMINAY AWEKEWA BEI

MANCHESTER United imeweka bei ya pauni milioni 30 kwa kiungo wa kati wa Mscotland, Scott McTominay, 27. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# MBAPPE SASA KUMILIKI KLABU KWAO UFARANSA

**PARIS,** Ufaransa

### ●●● Anakaribia kuwa mmiliki mpya wa Klabu ya Daraja la Pili ya Ufaransa ya...

NYOTA wa Real Madrid, Kylian Mbappe, anakaribia kuwa mmiliki mpya wa Klabu ya Daraja la Pili ya Ufaransa ya Stade Malherbe de Caen, kwa mujibu wa ESPN.

**Uchukuaji wa timu hiyo unapaswa kutangazwa mara moja, chanzo kilisema, na itamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kumiliki klabu ya soka barani Ulaya.**

Mchezaji huyo mpya wa Real Madrid, atawekeza takriban Euro milioni 15 kupitia mfuko wake wa Uwekezaji wa Coalition Capital ili kupata asilimia 80 ya mtaji wa klabu na pia atalipa sehemu ya deni la klabu.

Mbappe atachukua nafasi ya aliyekuwa na hisa nyingi hapo awali, Mfuko wa Uwekezaji wa Marekani Oaktree, ambao ulinunua asilimia 80 ya hisa za klabu hiyo mwaka 2020. Asilimia 20 iliyobaki inashikiliwa na Pierre Antoine Capton, rais wa sasa wa bodi ya usimamizi ya klabu.

Caen kwa sasa ipo Ligue 2 baada ya kushushwa daraja kutoka Ligi Kuu Mei 2019. Uhusiano kati ya Mbappe na Caen ni wa muda mrefu sana. Mnamo mwaka 2014, Mbappe alipokuwa na umri wa miaka 13, karibu asaini kujiunga nayo kabla ya kuchagua Monaco.


Chanzo hicho kilisema Caen inatarajiwa kumtaja rais mpya, Ziad Hammoud.

Hammoud ni rafiki wa karibu wa nahodha huyo wa Ufaransa na anasimamia kampuni yake ya haki za picha.

Washirika wengine wa karibu wa Mbappe wanaweza pia kuja kushikilia nyadhifa zingine kwenye klabu hiyo. Bado haijabainika ni kiasi gani cha fedha zake mwenyewe Mbappe atawekeza hatimaye na matarajio yake kwa klabu ni nini, chanzo kilisema.

Caen, jiji lililoko Kilomita 240 Magharibi mwa Paris, itaanza msimu wao wa Ligue 2 Agosti 17, mwaka huu dhidi ya Paris FC, siku tatu baada ya Mbappe kucheza mechi yake ya kwanza Real Madrid kwenye Kombe la Super Cup la Ulaya dhidi ya Atalanta siku moja kabla ya kuanza kwa kampeni ya LaLiga 2024 na safari ya kwenda Mallorca.

# DI MARIA: VITISHO VIMENIZUIA KUICHEZEA ROSARIO



**BUENOS AIRES,** Argentina

KIUNGO wa kati wa Argentina, Angel Di Maria, amesema alikuwa tayari kurejea katika klabu ya nyumbani kwao mji wa Rosario Central, lakini akabadilisha mipango yake kutokana na kuongezeka kwa vurugu zinazohusiana na dawa za kulevya katika eneo hilo na vitisho dhidi ya familia yake.

Di Maria ambaye alistaafu kuichezea Timu ya Taifa ya Argentina baada ya ushindi wao wa Copa America mapema mwezi uliopita, alisema miongoni mwa vitisho alivyotumiwa yeye na familia yake ni kusafirisha kichwa cha nguruwe kikiwa na risasi kwenye paji la uso kifurushi alichopokea dada yake na familia yake ambayo ilijumuisha tishio la kifo lililoandikwa dhidi ya binti yake.

"Kulikuwa na tishio lililofanywa katika mtaa wa wazazi wangu ambalo lilijitokeza hadharani na wakati huohuo lingine kwenye mali ya dada yangu ambalo halikuonekana kwa sababu dada na shemeji yangu walikuwa na hofu na hawakutoa taarifa," alisema Di Maria.

Di Maria mwenye umri wa miaka 36, alisema yeye na familia yake waliacha matumaini yao ya kurejea Central kufuatia vitisho vya Machi.

"Miezi hiyo ilikuwa ya kutisha," alisema, akiongeza kwamba "tuliweza tu kukaa pale na kulia kila usiku kwa kutoweza kutimiza ndoto hiyo ya kurejea katika klabu ambako nilicheza kwa mara ya kwanza."

Licha ya vitisho hivyo, Di Maria alisema alipokea shutuma kutoka kwa mashabiki wa Rosario kwa kutorejea nyumbani.

"Wale ambao hawaelewi, hawajiweki katika nafasi yangu kwa sekunde moja," Di Maria alisema. "Kwa sababu ni rahisi kuwadhulumu wengine kwenye mitandao ya kijamii bila kujiweka katika viatu vya mtu mwingine."



# Yoro azua hofu Manchester Utd

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inahofia mchezaji mpya, Leny Yoro, huenda akakaa nje ya uwanja kutokana na jeraha la kifundo cha mguu alilopata wakati wa mechi yao ya kirafiki dhidi ya Arsenal, chanzo kiliiambia ESPN.

Yoro alilazimika kutolewa nje katika kipindi cha kwanza cha kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Arsenal kwenye Uwanja wa SoFi mjini Los Angeles Jumamosi ikiwa ni mechi yake ya pili tu baada ya kuhama kutoka Lille.

Kijana huyo mwenye umri wa miaka 18, hajaweza kufanya mazoezi tangu siku hiyo na Jumanne alipigwa picha akiwa kwenye magongo na akiwa amevalia kiatu cha kujikinga mguu wake wa kushoto.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba wafanyakazi wa matibabu wa klabu bado wanakagua jeraha hilo.

United wamekataa kutoa maoni yao huku Kocha Erik ten Hag, akitarajiwa kuzungumzia hali hiyo katika mkutano na waandishi wa habari leo Alhamisi.

Yoro alikosa mechi ya kirafiki na Real Betis huko San Diego jana, Jumatano. Kumpoteza Yoro, ambaye alisajiliwa kwa pauni milioni 52 ni pigo kubwa kwa Ten Hag, ambaye alitarajia Mfaransa huyo angechukua nafasi ya Raphael Varane katika safu ya ulinzi. Varane amejiunga na Como ya Italia baada ya kuondoka Old Trafford kwa uhamisho wa bure mwishoni mwa msimu uliopita.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United bado wako sokoni kutafuta beki mwingine wa kati na wana nia ya kuwanunua Matthijs de Ligt wa Bayern Munich na Jarrad Branthwaite wa Everton.

Bayern wanataka pauni milioni 42 kwa De Ligt huku Everton wakitaka zaidi ya pauni milioni 70 kwa Branthwaite. United tayari wametuma ofa mbili rasmi kwa Branthwaite, ambazo zote zimekataliwa na Everton.

Pia, United wana wasiwasi kuhusu utimamu wa mshambuliaji Rasmus Højlund, ambaye alitolewa katika kipindi cha kwanza dhidi ya Arsenal baada ya kupata jeraha linaloshukiwa kuwa la msuli wa paja.

# Barcelona kwenda Olmo, kuachana na Williams

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeanza kukubali kwamba dili la kumnunua Nico Williams msimu huu wa majira ya joto linaonekana kuwa lisilowezekana na wanatathmini chaguzi zingine, pamoja na Dani Olmo, kwa mujibu wa ESPN.

Winga wa Athletic Club, Williams mwenye umri wa miaka 22, ndiye anayelengwa zaidi na Barca na rais Joan Laporta alipendekeza kuwa kipengele chake cha kuruhusiwa kuondoka cha euro milioni 58 wanaweza kukimudu, lakini sasa mambo yanaonekana kuwa magumu.

Vyanzo vya habari vinasisitiza kulipa kifungu hicho si shida, kwani Barca wana fedha, lakini hawawezi kuhakikisha kwamba Williams atasajiliwa na LaLiga mara moja.

Wamesalia kuvuka kikomo cha matumizi kilichowekwa na LaLiga na hadi pale watakapoleta fedha kupitia uhamisho au njia mpya za mapato, wanakuwa na kikomo cha kile wanachoweza kutumia kwenye ligi.

Shinikizo lililowekwa kwa Williams, ambaye aliichezea Hispania vema waliposhinda Euro 2024, kusalia Athletic - ambapo anacheza pamoja na kaka yake, Iñaki - kwa msimu mwingine, ni kocha wa Paris Saint-Germain kumtaka pia.

Vyanzo vya karibu na PSG vinaamini Williams anataka kujiunga na Barca, lakini timu hiyo ya LaLiga haiwezi kufanya makubaliano hivi sasa.

Hawajatoa ofa lakini wamefanya mazungumzo na kambi yake na wangemtaka msimu huu wa majira ya joto huku wakitarajia kujipanga upya kutokana na kumpoteza Kylian Mbappe.



Laporta alisema kutakuwa na "habari njema" hivi karibuni na hali ya kifedha ya Barca "imeboreka" wakati wa utambulisho wa kocha mpya, Hansi Flick wiki iliyopita.

Hata hivyo, Barca wanaamini kuwa makubaliano ya Olmo yanaweza kufikiwa zaidi, vyanzo vinasema.

## Mutale, Mukwala watema cheche

INATOKA UKURASA 24

na APR ya Rwanda, tiketi za mzunguko wa pili zimemalizika, huku zilizosalia ni za VIP B, VIP C na rangi ya machungwa ambazo nazo zimebaki chache.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amewataka mashabiki kununua tiketi kwenye majukwaa hayo, kwani mbali na mzunguko, tiketi za Platnum na VIP A, nazo zimemalizika.

## Kocha Gamondi akoshwa na ubora wa Mzize

INATOKA UKURASA 24

Kusini imewapa kitu wachezaji wake na wanataka kuendeleza pale walipoishia.

"Ilikuwa safari nzuri sana kwetu, ni maandalizi mazuri tumeyapata, kufanya mazoezi na kucheza michezo mitatu ya kirafiki na timu kubwa kama FC Augsburg na Kaizer Chief ni kipimo kizuri kwetu, hii itatusaidia kuelekea msimu ujao," alisema Gamondi.

Alisema kwa sasa anachofanya na wasaidizi wake ni kuimarisha baadhi ya maeneo ambayo waliona yana mapungufu wakiwa kwenye maandalizi yao Afrika Kusini.

Katika hatua nyingine, Gamondi, amewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi kwenye kilele cha tamasha lao la 'Wiki ya Mwananchi'.

Kilele cha tamasha hilo kitafanyika Jumapili ijayo kwa kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Red Arrows ya Zambia ukiwa ni mchezo wa mwisho kabla ya kukabiliana na Simba kwenye nusu fainali ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 8 kwenye uwanja huo.

# NYOTA SIMBA WAPANIA KUREJESHA HESHIMA

**Na Faustine Feliciane**

WACHEZAJI wakongwe wa klabu ya Simba, Nahodha Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na Shomari Kapombe, wamesema wamejiandaa kuhakikisha wanarejesha heshima klabuni hapo baada ya kutoka kapa kwenye ubingwa kwa misimu mitatu mfululizo.

Wakizungumza na gazeti hili jana, nyota hao wamesema usajili uliofanywa na viongozi wao umerejesha makali ya klabu hiyo kutokana na ubora wa wachezaji.

"Tumefanya maandalizi mazuri kambini, wachezaji wapya waliosajiliwa wameonyesha wana uwezo mkubwa pamoja kwa kushirikiana tunataka kurejesha heshima ya Simba kwa kutwaa ubingwa na kufanya vizuri zaidi katika mashindano ya kimataifa," alisema Zimbwe Jr.

Alisema benchi la ufundi la timu hiyo chini ya kocha Fadlu David, wamewapa mbinu mbalimbali na mipango ya kuhakikisha wanafanya vizuri.

"Tuna mchezo wa kirafiki Siku ya Simba Day, lakini tuna mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga, ni michezo ambayo itatupa mwanga wa kuanza vizuri msimu huu, tumejiandaa vizuri," alisema Zimbwe.

Aidha, Kapombe, aliwataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi siku ya tamasha la 'Simba Day' ili kuwaona wachezaji wao wapya.

"Msimu huu tunataka uwe wetu, viongozi wamefanya kazi kubwa na sasa ni sisi wachezaji, mashabiki waje kwa wingi kama kawaida yao kuona wachezaji wao," alisema Kapombe.

Tamasha la Simba Day limepangwa kufanyika Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo Simba itacheza mchezo wa kirafiki dhidi ya APR ya Rwanda.



Mchezaji kijana wa mchezo wa tenisi akirudisha mpira kwa mpinzani wake (hayupo pichani) wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Prince Dube ajitabiria mabao michuano ya CAF

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI mpya wa Yanga, Prince Dube amesema mabao yake mawili aliyofunga na 'asisti' moja kwenye mechi mbili za kirafiki dhidi ya TS Galaxy na Kaizer Chiefs zote za Afrika Kusini, yamemfanya kujiamini zaidi na kujitabiria kufunga mabao mengi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayotarajiwa kuanza Agosti 16, mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Dube amesema awali hakuwa vema kwani hakucheza soka kwa muda wa miezi sita, lakini michezo mitatu aliyocheza imemrudisha kwenye uwezo wake ule ambao alikuwa anauhitaji kuwa nao kabla ya mashindano kuanza.

Ingawa hakuonekana kucheza vema katika mechi ya kwanza Afrika Kusini dhidi ya FC Augsburg ya Ujerumani ambayo timu yake ilifungwa mabao 2-1, alipachika bao pekee katika mechi dhidi ya TS Galaxy na kufunga tena mechi dhidi ya Kaizer Chiefs na kutoa pasi iliyozaa bao kwa Clement Mzize, Yanga ikiivurumisha timu hiyo mabao 4-0.

"Nimefurahi sana kwa michezo mitatu ambayo tumecheza Afrika Kusini, imenisaidia sana, imenirudisha kwenye kiwango changu kile ninachokifahamu, nilikaa muda mrefu bila kucheza soka la kiushindani, nimecheza mechi na timu za nje ya nchi, unajua ukicheza mechi kubwa kama hizi ina maana unaweza kucheza na timu yoyote kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na ukafunga mabao, nadhani hii imenifungulia milango, nahitaji kufunga mabao mengi mechi za kimataifa na nahitaji kuisaidia Yanga kupata mafanikio," alisema Dube.

Aidha, aliwashukuru wanachama na mashabiki wa klabu hiyo ambao wamekuwa wakimtumia salamu nyingi za kumpongeza ambazo nazo zinampa morali wa kuzidi kufanya mazoezi kwa bidii kuweza kuisaidia timu yao hasa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo alisema hakuwa anapata nafasi ya kushiriki.

"Kwenye ligi hakuna anayeweza kuhoji uwezo wangu, lakini Ligi ya Mabingwa Afrika nina muda mrefu sana sijacheza, nataka nionyeshe uwezo wangu huko, nimekuja Yanga kwa sababu hiyo tu, hivyo wanachama na mashabiki wasiwe na wasiwasi na mimi, nikishirikiana na wenzangu hakuna kitakachoshindikana," alisema mchezaji huyo raia wa Zimbabwe.

Alisema kitu kingine ambacho amebahatika kukikuta Yanga ni kucheza na wachezaji wawili anaowakubali, Clatous Chama na Stephane Aziz Ki, ambao amesema watamsaidia sana kwenye kazi yake ya kupachika mabao.

"Nimefurahi sana kucheza na wachezaji hawa, ni wachezaji wakubwa, ninajifunza vitu vingi kutoka kwao, na mimi nipo nao ili kuongeza kitu kwenye timu, najiona kama nina bahati ya kupata nafasi ya kucheza na wachezaji kama hawa," alisema Dube.

# Michezo

Alhamisi Agosti 1, 2024

Nipashe




Yoro azua hofu Man Utd UKURASA 22



Mshambuliaji mpya wa Simba, Deborah Fernandez, muda mfupi baada ya kuwasili uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, akiwa na timu hiyo wakitokea Misri walipokuwa wameweka kambi kujiandaa na msimu mpya. **PICHA: SIMBA**

## Gamondi akoshwa na ubora wa Mzize

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema mshambuliaji wa timu hiyo, Clement Mzize ameonyesha kuongeza kiwango chake kwa kiasi kikubwa na kumtabiria kufanya vizuri msimu ujao.

Akizungumza akiwa jijini Dar es Salaam baada ya kurejea kutoka Afrika Kusini walipoenda kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya pamoja na kushiriki mashindano ya Toyota Cup, Gamondi, alisema mmoja wa wachezaji aliyemkosha kutokana na uwezo aliouonyesha ni Mzize.

"Mzize, naamini atafanya makubwa zaidi msimu ujao, ameonyesha uwezo mkubwa, amekuwa na kasi na utulivu golini, amekuwa na uwezo mkubwa, anaweza akafanya vizuri zaidi ya msimu uliopita," alisema Gamondi.



Aidha, alisema wataendelea na mazoezi yao Avic Town, Kigamboni kwa ajili ya mechi yao ya kirafiki katika kilele cha Wiki ya Wananchi watakapocheza na Red Arrows ya Zambia.

"Tutaendelea na maandalizi yetu, kuna mechi mbili katika siku chache zijazo, mchezo kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi na mchezo dhidi ya Simba, tunafanya maandalizi ya michezo hii miwili," alisema Gamondi.

Gamondi, alisema michezo mitatu waliyocheza Afrika

INAENDELEA UKURASA 23

# NYOTA MUTALE, MUKWALA WATEMA CHECHE SIMBA

## ●●● Wawaambia mashabiki wasubiri kuona timu mpya, yamaliza tiketi za 'ubaya ubwela' huku...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI tiketi za jukwaa la mzunguko kwa ajili ya kuingia katika kilele cha tamasha la Simba Day Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa lililopewa kaulimbiu ya 'Ubaya Ubwela, wachezaji wapya Joshua Mutale na Steven Mukwala wamewaambia mashabiki wa timu hiyo kuwa wataishuhudia timu tofauti na ile waliyoiona msimu uliopita.

**Nyota hao walisema msimu huu Simba ina wachezaji wanaocheza soka safi na la kuburudisha huku wakiwa na uwezo mkubwa, ari na nguvu, pamoja na benchi bora la ufundi lenye mbinu nzuri za ufundishaji chini ya Kocha Fadlu Davids.**

Wachezaji hao wamewataka mashabiki kwenda uwanjani kuona soka safi la burudani, pamoja na ushindi usiokuwa na shaka.

Kikosi hicho kimewasili jana jijini Dar es Salaam kutoka nchini Misri ambako kiliweka kambi kwa takriban wiki tatu kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano.

Mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Mukwala, alisema mechi yao ya mwisho ilieleza kila kitu, kwani walicheza jinsi ambavyo kocha wao siku zote alikuwa anataka wacheze na waliweza kufanikiwa kutokana na kuwa fiti tofauti na michezo miwili iliyopita.

"Mechi ya mwisho ilieleza kila kitu, ilikuwa ngumu kuliko zote tulizocheza, timu kutoka Saudi Arabia haikuwa rahisi, lakini tulipambana na kuweza kushinda, nawaahidi wanachama na mashabiki wa Simba wataona mchezo mzuri sana kila tutakapocheza, wataona kitu tofauti na walichokiona msimu uliopita, tunajua nini wanataka na tuwape hicho wanachohitaji," alisema mshambuliaji huyo raia wa Uganda aliyesajiliwa kutoka klabu ya Asante Kotoko ya Ghana.

Katika mechi ya mwisho, Jumatatu usiku, Simba ilicheza dhidi ya Al Adalah ya Saudi Arabia, Uwanja wa New Suez Canal nchini humo na kushinda mabao 2-1, ambao yalifungwa na Mukwala pamoja na Mutale.

Aidha, Mutale kwa upande wake alisema kwa sasa wapo katika utimamu wa miili kwa asilimia 90 na ndicho kilichofanya wapate ushindi katika mchezo wao wa mwisho huku akisema sasa wapo tayari kwa ajili ya Simba Day pamoja na msimu mpya wa mashindano, licha ya kwamba Kocha Fadlu bado anafanya marekebisho ya hapa na pale.

"Kwa sasa tupo kwenye asilimia 90 ya kiwango cha utimamu wa mwili, mazoezi yalikuwa mazuri na magumu, mchezo wetu wa tatu umeonyesha tayari tupo kamili, tulikuwa tunakaba wote, tunakimbia kwa kasi, kukaa kwenye maeneo sahihi kwa wakati sahihi na hata wakati mwingine tulikuwa tunapigiana pasi ndefu kila upande wa uwanja haraka haraka huku tukikimbilia eneo la adui kiasi cha kuwachanganya wapinzani na hata bao la pili lilofunga lilipatikana kwa mtindo huo.

Nadhani sasa tupo tayari kwa Simba Day na msimu mpya, najua mashabiki wetu watatupokea vizuri kutokana na hiki ambacho tunawapelekea uwanjani," alisema Mutale, winga mpya aliyesajiliwa kutoka Power Dynamos ya Zambia.

Wakati hayo yakiendelea kuelekea kwenye Tamasha la Simba Day ambapo timu hiyo itacheza

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002